# ATHARI ZA KIMOFOFONOLOJIA ZA LUGHA YA KIRUNDI KATIKA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI KAMA LUGHA YA PILI KWA WANAFUNZI WA JAMIILUGHA YA KIRUNDI

**JEAN BIZIMANA**

**TASNIFU HII ILIWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI-ISIMU KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2022**

## UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii yenye mada: ***Athari za Kimofofonolojia za Lugha ya Kirundi Katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili kwa Wanafunzi wa Jamiilugha ya Kirundi***na kupendekeza kwamba tasnifu hii imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili (M.A. Kiswahili -Isimu) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

……..…………………………….

Dkt. Zelda Elisifa

(Msimamizi)

Tarehe…………………………….

## TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, **Jean Bizimana**, nathibitisha kwamba tasnifu hii yenye mada ya ***Athari za Kimofofonolojia za Lugha ya Kirundi Katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili kwa Wanafunzi wa Jamiilugha ya Kirundi***ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuhudhurishwa na wala haitahudhurishwa kwenye chuo kikuu kingine kwa lengo la kutunukiwa shahada kama hii.

……………………………

Saini

Jean Bizimana

………………………………

Tarehe

## HATIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile sehemu yoyote ya tasnifu hii, kwa njia yoyote ile kama vile kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine, bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba ya mwandishi.

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa mke wangu mpendwa, Floride Nahishakiye, kwa kunitia moyo wa kuendelea na masomo yangu.

## SHUKURANI

Kwanza kabisa, namshukuru Mungu kwa kunipa afya na uwezo wa kuifanya kazi hii. Mungu apewe sifa.

Shukurani za dhati kabisa zimwendee Dkt Zelda Elisifa, msimamizi wangu. Ametumia muda wake mwingi na amenivumilia katika kusimamia, kusahihisha na kutoa msaada wa maelekezo mpaka kazi ikafika katika hatua hii. Ninamshukuru sana kwa ushauri na upendo wake. Nasema asante sana.

Ninapenda pia kuwashukuru waalimu wote wa Idara ya Isimu na Lugha, katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa mchango wao wa kitaaluma walionipa. Baadhi yao ni Mwl. Bakari Kombo Bakari, Dkt. Nasra Habibu, Dkt. Hadija Jilala na mratibu wetu Dkt. Omary Maguo. Mungu awabariki wote. Pia ninakishukuru Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hasa Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii kwa kutupa fursa ya kusoma tukiwa nchini Burundi.

Aidha ningependa kumshukuru mke wangu, Floride NAHISHAKIYE, na watoto wangu, Eunice NIYOKWIZERWA, Béni Bilga MPUNDU, Déborah NINZIZA MAHORO, Jédidiah MWIZIGIRWA, Chérubin MUGISHA, Esther Shammah INGABIRE, Joshua Blessed MUTABAZI, Ange Naomie ITEKA, kwa kunivumilia na kuniombea wakati wa kujiendeleza kielimu na kufanya kazi hii ya utafiti.

Siwezi kukamilisha shukrani zangu bila kuwashukuru watafitiwa wote ambao wameniwezesha kupata taarifa za utafiti huu, na wote walioshiriki katika kufanikisha kazi hii kwa namna moja au nyingine. Shukrani zangu za dhati ziwafikie na kazi hii iwe tuzo kwao.

## IKISIRI

Utafiti huu ulitathmini ***Athari za Kimofofonolojia za Lugha ya Kirundi Katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili kwa Wanafunzi wa Jamii lugha ya Kirundi katika baadhi ya vyuo vikuu***. Malengo mahususi katika utafiti huu ni (1) Kubainisha athari za kimofofonolojia ya Kirundikatika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi; (2) Kutathmini viwango vya utamalaki wa aina mbalimbali za athari za Kimofofonolojia za Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi., na (3) kubainisha juhudi za walimu kubaini na kukabiliana na aina hizi za athari. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Linganishi. Ili kufikia malengo yake, wanafunzi mia moja wa vyuo vikuu vitatu walihusishwa pamoja na wahadhiriwa Kiswahili wanane. Michakato ya usampulishaji iliyotumiwa ni usampulishaji usio nasibu na usampulishaji nasibu. Mbinu za kukusanyia data zilikuwa hojaji, jaribio la umilisi na ushuhudiaji. Uchanganuzi wa data ulionyesha kuwa athari za kimofofonolojia zinazoibuka katika kazi za Kiswahili za wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi wanaojifunza Kiswahili yalihusu uchopekaji, udondoshaji na matumizi ya fonimu mbadala. Aghalabu athari za kimofofonolojia zilizodhihirika zilisababishwa na uhawilishaji wa L1 ya mwanafunzi kwa kuhamisha baadhi ya kanuni za kiisimu za L1 hadi L2. Katika kuangazia mbinu za kutumiwa na walimu ili kuwasaidia wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama L2, walimu watafititiwa walibaini mbinu za hatua kwa hatua; yaani stadi ya kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.

**Maneno Makuu:** *Kimofofonolojia*, *Fonimu*, *Uchopekaji*

# YALIYOMO

UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI ........ ii
TAMKO LA MTAHINIWA ........ iii
HATIMILIKI ........ iv
TABARUKU ........ v
SHUKURANI ........ vi
IKISIRI ........ vii
YALIYOMO ........ viii
ORODHA YA MAJEDWALI ........ xii
ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ........ xiii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ........ 1**

1.1 Usuli wa Mada ........ 1
1.1.1 Fasili ya Lugha ya Kwanza (L1) na Lugha ya Pili (L2) ........ 1
1.1.2 Dhana ya Uamiliaji na Ujifunzaji Lugha ........ 3
1.2 Tatizo la Utafiti ........ 4
1.3 Malengo ya Utafiti ........ 4
1.3.1 Lengo Kuu ........ 5
1.3.2 Malengo Mahususi ........ 5
1.4 Maswali ya Utafiti ........ 5
I.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 5
I.6 Upeo na Mipaka ........ 6
1.7 Hitimisho la Sura ya Kwanza ........ 7

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA . 8**

2.1 Utangulizi ........ 8

2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi ........ 8

2.2.1 Dhana ya Mofofonolojia ........ 9

2.2.2 Sarufi Majumui na Uamiliaji L2 ........ 9

2.2.3 Athari za L1 katika L2 ........ 12

2.2.4 Tafiti Zihusuzo Athari za Lugha Nyingine za Kibantu katika Lugha ya Kiswahili ........ 15

2.2.5 Kazi Mahususi Zinazohusu Athari za Lugha ya Kirundi kwenye L2 ........ 21

2.3 Pengo la Utafiti ........ 23

2.4 Kiunzi cha Nadharia ........ 24

2.4.1 Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ........ 24

2.4.2 Hatua za Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ........ 25

2.4.3 Sababu za Kuchagua Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ........ 26

2.5 Hitimisho la Sura ya Pili ........ 26

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........ 27**

3.1 Utangulizi ........ 27

3.2 Usanifu wa Utafiti ........ 27

3.3 Eneo la Utafiti ........ 28

3.4 Sampuli ........ 28

3.5 Usampulishaji ........ 30

3.6 Mbinu za Utafiti ........ 31

3.6.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 32

3.6.1.1 Hojaji ........ 32

3.6.1.2 Jaribio la Umilisi ........................................................................ 32

3.6.1.3 Ushuhudiaji ........................................................................ 33

3.7 Mkabala wa Uchambuzi wa Data ........................................................................ 33

3.8 Maadili ya Utafiti ........................................................................ 34

3.9 Hitimisho la Sura ya Tatu ........................................................................ 34

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ........................................................................ 36**

4.1 Utangulizi ........................................................................ 36

4.2 Uwasilishaji wa Data ........................................................................ 36

4.3 Athari za Kimofofonolojia za Kirundi (L1) Katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili (L2) ........................................................................ 37

4.3.1 Uchopekaji ........................................................................ 38

4.3.1.1 Uchopekaji wa Irabu /u/ na /i/ ........................................................................ 39

4.3.1.2 Uchopekaji wa Sauti /h/ ........................................................................ 42

4.3.1.3 Uchopekaji wa Viyeyusho /j/ , /w/ ........................................................................ 43

4.3.2 Udondoshaji wa konsanti /h/ ........................................................................ 45

4.3.3 Matumizi ya Ubadala ........................................................................ 47

4.3.3.1 Matumizi ya /β/ badala ya /b/ ........................................................................ 49

4.3.3.2 Matumizi ya ‘c’ badala ya ‘ch’ ........................................................................ 50

4.3.3.3 Matumizi ya Konsonanti /g/ badala ya /ɤ/ ........................................................................ 50

4.3.3.4 Matumizi ya Konsonanti /r/ badala ya /l/ ........................................................................ 52

4.3.3.5 Matumizi ya Konsonanti/z/ badala ya /ð/ ........................................................................ 53

4.3.3.6 Matumizi ya /s/ badala ya /ɵ/ ........................................................................ 54

4.3.3.7 Matumizi ya Konsonanti /f/ badala ya /ɵ/ ........................................................................ 55

4.4 Juhudi za Walimu Kubaini na Kukabiliana na Athari kimofofonolojia za Kirundi katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama L2. .................................... 58
4.4.1 Usikilizaji .................................................................................. 60
4.4.2 Stadi ya Uzungumzaji au Maongezi ............................................ 61
4.4.3 Stadi ya Usomaji ........................................................................ 62
4.4.4 Stadi ya Uandishi ....................................................................... 63
4.5 Hitimisho la Sura ya Nne ............................................................... 64

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........... 66**
5.1 Utangulizi .................................................................................... 66
5.2 Muhtasari .................................................................................... 66
5.3 Hitimisho la Sura ya Tano............................................................. 69
5.4 Mapendekezo ............................................................................... 70
5.4.1 Mapendekezo ya kiutekelezaji kwa watunga muhtasari wa somo, watunga sera za lugha katika elimu, kwa walimu....................................... 70
5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti Zitakazokuja.......................................... 71

**MAREJELEO..... .......................................................................... 72**

**VIAMBATISHO.. .......................................................................... 78**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na.3.1: Mgawanyo wa watafitiwa kwa kigezo cha makundi na maeneo wanayotoka ........ 30

Jedwali Na. 4.1: Jumla ya Aina za Athari ........ 38

Jedwali Na.4.2: Idadi ya Athari za Kimofofonolojia kutokana na Uchopekaji ........ 39

Jedwali Na.4.3: Mifano ya Uchopekaji wa Irabu /u/ ........ 40

Jedwali Na. 4.5: Mifano ya Uchopekaji wa Sauti /h/ ........ 42

Jedwali Na. 4.6: Mifano ya Uchopekaji wa Kiyeyusho /j/ Kiothografia ........ 44

Jedwali Na. 4.7: Mifano ya Uchopekaji wa Kiyeyusho /w/ Kiothografia ........ 45

Jedwali Na. 4.8: Idadi ya Hali ya Utokeaji wa Udondoshaji wa /h/ ........ 46

Jedwali Na.4.9: Mifano ya Udondoshaji wa /h/ ........ 47

Jedwali Na. 4.10 : Aina na Idadi ya Athari za Matumizi ya Konsonanti Mbadala ........ 48

Jedwali Na. 4.12: Mifano ya Matumizi ya /β/ badala ya /b/ ........ 49

Jedwali Na. 4.12: Mifano ya Matumizi ya ‘c’ badala ya ‘ch’ Kiothografia ........ 50

Jedwali Na. 4.13: Mifano ya Kiothografia ya Matumizi yaKonsonanti /g/ Badala ya /ɣ/ ........ 51

Jedwali Na.4.14: Mifano ya matumizi ya Konsonanti/r/ badala ya /l/ ........ 52

Jedwali Na. 4.15: Mifano ya Kiothografia ya Matumizi ya /z/ badala ya /ð/ ........ 53

Jedwali Na. 4.16: Mifano ya Matumizi ya Konsonanti/s/ badala ya /ɵ/ ........ 54

Jedwali Na.4.17: Mifano ya Matumizi ya Konsonanti/f/ badala ya /ɵ/ ........ 55

Jedwali Na. 4.18: Mbinu za walimu kubaini na kukabiliana na athari za mofofolojia ........ 59

## ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| I | Irabu |
| K | Konsonanti |
| L1 | Lugha ya kwanza |
| LL | Lugha Lengwa |
| L2 | Lugha ya pili |
| [ ] | Mabano ya fonetiki |
| / / | Mabano ya fonimu |
| {} | Mabano ya mofu |
| $ | Mpaka wa silabi |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Suala la athari linajitokeza pale ambapo lugha mbili tofauti au zaidi zinapozungumzwa. Hapo kuna uwezekano mkubwa sana wa kuathiriana katika nyanja ya ujifunzaji pale ambapo mwanafunzi anapotak a kukujifunza lugha ya pili (L2). Athari za lugha mama zinaweza kuwa mfanano au utofauti baina ya lugha hizi mbili katika nyanja mbalimbali za kiisimu, kiutamaduni na kijamii. Katika nyanja ya isimu, athari hizi hasa huweza kujitokeza katika matamshi, sarufi na hata lafudhi. Corder (1967), akizungumzia mwingiliano wa lugha na mapokezi ya L2, anasema kuwa makosa katika L2 yanaonyesha hali fulani ya matatizo aliyo nayo yule anayejifunza L2 kutokana na kuhamisha sifa fulani za L1 hadi kwenye L2. Kazi za Onyango (1997), Ndung'u (1999) na Mutugu (2001) ni mifano inayoonyesha kuwa wengi mwongoni mwa wanaojifunza Kiswahili kama L2 hukumbwa na matatizo katika ujifunzaji wake kama L2. Lado (1957) anadai kwamba makosa ya ujifunzaji ni ishara ya matatizo waliyonayo wanaojifunza lugha kuhusu vipengele fulani vya lugha hiyo. Kulingana na Richards na Wenzake, wakinukuliwa na Njoroge (1996), kosa hurejelea matumizi ya kipashio cha kiisimu kwa njia ambayo mzawa wa lugha husika angeona kina kasoro au kinaonyesha kutoimudu lugha kwa ukamilifu.

### 1.1.1 Fasili ya Lugha ya Kwanza (L1) na Lugha ya Pili (L2)

Kama anavyofasili Massamba (2016), L1 ni lugha ambayo alilelewa na kukua nayo mzungumzaji ambaye anajua na kutumia lugha mbili au zaidi. Sterm (1983) anasema kwamba L1 ni lugha ambayo mtoto hupata kutoka kwa mama yake mzazi angali mchanga; ni ile lugha ambayo mzungumzaji hutanguliza kuiongea maishani mwake,

yaani ile lugha inayotangulia kumwezesha kuwasiliana na wenzake kisauti, kabla ya lugha nyinginezo. Kwa mujibu wa Msanjila (2009), lugha mama ni L1 anayojifunza mtoto baada ya kuzaliwa.

UNESCO (2003) wanaeleza kwamba L1 ni ile lugha ambayo mjifunzaji anajifunza kwanza kabla ya lugha nyingine ambayo inajulikana kama lugha mama ya mjifunzaji. Aidha, UNESCO (weshatajwa) wanaendelea kueleza kwamba lugha hii ni lugha ambayo inafahamika zaidi na hutumika zaidi na wazungumzaji wanaohusika na lugha hiyo kuliko lugha nyingine ambazo wajifunzaji hao wanachangamana nazo. Kwa ujumla, fasili zote hizi za L1 zinafanana na hivyo tunaweza kusema kwamba L1 ni lugha ambayo mtu anaitumia kama lugha yake tangu utotoni mwake kutoka kwa mlezi wake wa msingi. Hivyo huzaliwa na kuikuta jamii yake na lugha hiyo na kuitumia katika mazingira yake kimawasiliano.

Kwa upande mwingine, L2 ni ile lugha ambayo mtu anajifunza baada ya ile ya awali. Massamba (2016) anaeleza kwamba L2 ni lugha anayojifunza mtu baada ya kujifunza L1 yake. Kwa mujibu wa Stern (1983), L2 ni ile lugha ambayo mtu hujifunza mbali na lugha mama yake. Aidha, Saville-Troike (2006) amefasili dhana ya L2 kwa mapana zaidi, licha ya kukubali kwamba ni lugha ambayo huja baada ya mtu tayari kuwa na lugha mama. Yeye alienda mbali zaidi kwa kuhusisha L2 na nguvu, majukumu na dhima ya lugha hiyo katika jamii.

Kutokana na fasili hizi, ni dhahiri kwamba lugha ya Kiswahili ni L2 kwa Warundi walio wengi hasa waishio vijijini kwani hujifunza lugha hii wakiwa tayari wana lugha yao ya Kirundi kama L1.

### 1.1.2 Dhana ya Uamiliaji na Ujifunzaji Lugha

Dhana ya uamiliaji lugha imefasiliwa na Krashen na Tracy (1981) kuwa ni mchakato unaotokea katika nafsi iliyofichika akilini mwa mtu ambayo ndiyo imwongozayo kuongea au kuandika kwa urahisi. Hivyo wao wanaona kuwa uamiliaji hujitokeza kwa mtu katika hali ya ung'amuzi bwete pasipo muhusika mwenyewe kujitambua. Garman na Fletcher (1986) wanasema kuwa uamiliaji lugha hautokei katika ombwe kwani kadiri watoto wanavyoamili lugha wanaamili mfumo wa ishara ambazo zinaonesha uhusiano muhimu katika nyanja ya ubongo na nyanja ya jamii katika maisha.

Na katika ujifunzaji lugha, Krashen na Tracy (wameshatajwa) wanadai kuwa ni mchakato wa kiufahamu wa kiakili au utambuzi wa nafsi unaojionesha katika kujifunza sheria na kanuni na miundo ya lugha. Hivyo basi wao wanaona kuwa ujifunzaji ni tukio la kiutambuzi, yaani mtu anakuwa anafahamu au anatambua kuwa anajifunza lugha hivyo na atapaswa kuzingatia kanuni na muundo wa lugha. Mtalaam mwingine ambaye anaonesha kukubaliana na akina Krashen na mwenzake ni Gleason (1989) ambaye anaona kuwa uamiliaji lugha ni sawa na tukio linalotokea katika ung'amuzi bwete wakati ujifunzaji hutokea katika ung'amuzi tambuzi. Katika kuthibitisha hilo anasema kuwa ujifunzaji lugha unazingatia kujua vipengele muhimu vya lugha ambavyo si lazima kuvifuata au kuvijua katika uamiliaji lugha bali vinakuja vyenyewe pasipo utambuzi au pasipokujua. Vipengele hivyo ni fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na pragmatiki.

Nchini Burundi lugha ya Kiswahili hufufundishwa kama somo la lazima katika shule za msingi, sekondari na vyuo. Hivyo katika utafiti huu kuchunguza athari za

kimofofonolojia za lugha ya Kirundi zinazojitokeza katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi wa jamii lugha ya Kirundi pamoja na kuibua mbinu za kukabiliana na athari hizo, kutarahisisha ujifunzaji wa Kiswahili na kuendeleza hadhi ya Kiswahili.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Athari ya lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili haiepukiki. Kazi za wataalam mbalimbali (mf. Haroon, 1998; Otiende, 2013, Mashaka, 2015; Nyanda, 2015) zimeonyesha kwamba kuna athari za L1 katika ujifunzaji wa L2. Tafiti hizo ziliegemea ama upande wa fonolojia, mofonolojia, sintakisia au semantiki. Watafiti hao walitafiti athari kutokana na lugha za asili katika ujifunzanji wa Kiswahili sanifu na wamebainisha athari za kimatamshi, kimofolojia na kisintaksia. Hata hivyo, tafiti hizi hazikuangazia athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi zinazojitokeza katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi. Kwa muktadha huo, utafiti huu ulinuia kutathmini athari za kimofofonolojia za kirundi kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi wanaojifunza Kiswahili kama L2, ili kubaini aina za athari hizo, kutathmini viwango vya utamalaki wa aina mbalimbali za athari hizo na kubainisha mbinu za walimu kubaini na kukabiliana na athari za kimofofonolojia za Kirundi L1 ya wanafunzi.wajifunzao Kiswahili kama L2.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo ya aina mbili: lengo kuu na malengo mahususi. Malengo hayo yameainishwa hapa chini kama ifuatavyo.

; (2) na (3)

### 1.3.1 Lengo Kuu

Kutathmini athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi katika baadhi ya Vyuo Vikuu vya Burundi.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

i) Kubainisha athari za kimofofonolojia za Kirundikatika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi.

ii) Kutathmini viwango vya utamalaki wa aina mbalimbali za athari za Kimofofonolojia za Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi.

Kubainisha juhudi za walimu kubaini na kukabiliana na aina hizi za athari

## 1.4 Maswali ya Utafiti

i) Ni kwa namna gani Kirundi inavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi?

ii) Ni kwa viwango gani vya utamalaki wa athari mbalimbali za Kirundi L1 katika ujifunzaji wa Kiswahilikama L2 hutokea kwa wanafunzi hao ?

iii) iii) Kuna juhudi gani za walimu wa Kiswahili katika kubaini na kukabiliana na aina hizi za athari ?

## I.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utatoa mchango mkubwa wa kitaalamu na kinadharia katika isimu. Kwa upande wa taaluma, utafiti huu utasaidia katika utafiti juu ya athari za mofofonolojia ya lugha ya Kirundi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 kwa sababu hadi sasa hakuna utafiti uliofanyika juu ya mada hii. Hivyo utawasaidia wadau wa

Kiswahili kama vile wanafunzi, walimu, Maafisa Elimu kuwa na uelewa juu ya mada hiyo ya utafiti na hivyo kuweza kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Kupitia utafiti huu, jamii itakuwa na ufahamu juu ya athari za kimofofonolojia za Kirundi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 na hivyo kushirikiana kwa ukaribu na wadau wa elimu kuhamasisha ujifunzaji wa Kiswahili.

Utafiti huu utawafaa wanazuoni na wataalamu wa isimu kuelewa kwa undani zaidi juu ya athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi katika kujifunza lugha ya Kiswahili  nchini Burundi.

Utafiti huu utakuwa na utaendelea kuwa kichocheo cha tafiti nyingine kuhusu kuathiriana kwa lugha mama na Kiswahili nchini Burundi, Afrika na dunia nzima kwa ujumla.

## I.6 Upeo na Mipaka

Kazi hii iliangaza athari za mofofonolojia za Kirundi kama L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2. Utafiti huu utajikita kwenye (i)  lugha fasaha ya madarasani pekee na (ii) vipengele vya kiisimu vya mofofonolojia tu. Vipengele vya kiisimu vinginevyo kama sintaksia, semantiki au pragmatiki havikuhusishwa. Aidha, utafiti huu ulilenga athari mbalimbali za kimofofonolojia ya kimatamshi na ya kimaandishi ya Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wanaoongea Kirundi.Athari zilizoshughulikiwa ni za kipengele cha kimofofonolojia ambacho kinahusu mofolojia na fonolojia ambavyo vikiunganishwa ni mofofonolojia na zinahusu sauti na uundaji wa maneno kutokana na sauti hizo. Umilisi wa sauti za lugha yoyote ni njia mwafaka

ya kuelewa fonolojia ya lugha mahsusi. Taaluma zingine za isimu hazitashughulikiwa katika utafiti huu. Utafiti huu uliwashirikisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka vyuo vikuu vitatu yaani Chuo kikuu cha Maziwa Mapana (Universite des Grands lacs, UGL), Chuo Kikuu cha busara ya Afrika (Universite Sagesse d'Afrique, USA) na Chuo Kikuu cha Mwaro ( Universite de Mwaro, UM) nchini Burundi.

## 1.7 Hitimisho la Sura ya Kwanza

Katika sura hii ya kwanza, tumeeleza usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti huu, na upeo na mipaka ya utafiti huu. Sura inayofuata itahusika na tathmini ya tafiti tangulizi.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Ingawa mengi yameandikwa kuhusu jinsi lugha nyingi zinavyoathiri Kiswahili na hata lugha hizo kuathiriwa na Kiswahili, ikumbukwe kuwa kila lugha ina muundo na sifa zake. Kwa hivyo, kila lugha huathiri lugha nyingine kwa njia yake ya kipekee. Zaidi ya hayo, yaliyoandikwa pia hutofautiana. Katika sura hii tutarejelea mapitio ya kitaaluma ya kazi tangulizi kuhusu mada hii. Aidha, kiunzi cha nadharia kitatabainishwa ndani ya sura hii ambayo itahitimishwa na pengo la utafiti.

## 2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Cozby na Bates (2012), wanaeleza kwamba mapitio ya maandiko ni nakala zote zilizoelezea kwa ufupi tafiti zilizokwisha fanyika katika eneo fulani. Kupitia maandiko ni mchango unaohusu uchunguzi wa kina kwa maandiko yaliyotangulia eneo fulani la taaluma. Kazi hizi zinaweza kuwa vitabu, makala au majarida.

Lengo la kusoma mapitio ya kazi nikuchambua tafiti ili kubaini pengo lililopo, ili kumpa mtafiti changamoto ya kutaka kuziba pengo la kitaaluma linalohitaji kujazwa kikamilifu au kwa kiasi fulani. Mapitio ya kazi mbalimbali hutoa mwongozo kwa mtafiti. Mchango mzima wa upitiaji wa kazi mbalimbali hufungamana na kanuni zake kama kuhakiki, kujadili na kutoa maoni ya utafiti ili kuboresha utafiti unaokusudiwa kufanywa. Hivyo, utafiti huu unaendelea na kazi zilizoandikwa na wataalamu mbalimbali.

### 2.2.1 Dhana ya Mofofonolojia

Neno mofofonolojia limeundwa na maneno mawili mofolojia na fonolojia. Maneno haya huwakilisha viwango tofauti katika usomaji wa isimu. Fonolojia ni utanzu wa isimu ambao unahusu matumizi ya sauti katika lugha mahususi. Mofolojia ni utanzu wa isimu unaojishughulisha na uchunguzi, uchambuzi na ufafanuzi wa maumbo ya maneno katika lugha mahususi. Maneno haya mawili yanahusiana kwa kuwa kanuni za kifonolojia zinaweza kutumiwa kuelezea maumbo ya kimofolojia, kanuni hizi si za kueleza maumbo tu bali pia huweza kubadili umbo la neno; yaani umbo la ndani na umbo la nje. Kwa hivyo maneno haya yakiunganishwa yatakuwa mofofonolojia. Massamba (2010) akimrejelea Martnet (1965) anafafanua kwamba, istilahi ya mofofonolojia ilipendekezwa mara ya kwanza na Trubetzkoy (1929). Trubetzkoy alitumia istilahi hii kwa maana ya tawi la isimu linaloshugulikia matumizi ya mofolojia katika kueleza baadhi ya tofauti za kifonolojia ambazo zisingewezekana kuelezewa kwa kutumia data za kifonolojia au kifonetiki peke yake.

### 2.2.2 Sarufi Majumui na Uamiliaji L2

Kwa mujibu wa Chomsky (1976), sarufi majumui ni mfumo wa kanuni na sheria ambazo ni msingi wa lugha za binadamu. Mwasisi wa nadharia hii ni Noam Chomsky. Msingi wa nadharia hii ni kwamba binadamu anapozaliwa anakuwa na maarifa asilia ambayo humsaidia katika ujifunzaji lugha; mambo ya ndani na nje ambayo husaidia katika uamiliaji wa lugha. Maarifa haya hupatikana pale tu binadamu anapozaliwa kwani huwa na kifaa cha uamiliaji lugha ambacho kina kanuni majumui na kanuni badilifu ambazo hukutana na tajiriba (uwezo wa jamii katika lugha) na kusababisha uamiliajli lugha kutokea. Waamiliaji wa L1 huwa na maarifa asilia ambayo huwawezesha kuiamili lugha yao kwa kutumia maarifa hayo.

Hivyo maarifa hayo yameamshwa na tajiriba ambayo mjifunzaji anaikuta katika jamii iliyomzunguka na hatimaye kukutana na maarifa asilia katika kifaa cha uamiliaji lugha hatimaye kuzalisha sarufi mahsusi ya lugha husika. Waamiliaji wa L2 wanakuwa na L1 ambapo sifa za sarufi majumui bado humwezesha kuamili L2, kwani kanuni badilifu na kanuni majumui zilizojengwa kwa misingi ya L1 hutumika katika kuamilia L2

Wataalamu mbalimbali wameweza kujadili juu ya uwezo wa sarufi majumui wa kuwa kifaa wezeshi cha kujifunza L2. Flyn (1984) anaeleza kuwa kifaa cha uamiliaji L1 kitahusika na mchakato wa ujifunzaji L2. Anaendelea kusema kanuni badilifu za L1 na L2 zikiwa sawa ujifunzaji utakuwa rahisi kwa sababu mjifunzaji wa L2 ana uwezo wa kuhusisha miundo wakati kanuni hizo zikitofautiana kati ya L1 na L2 ni vigumu kujifunza. Flyn (ameshatajwa) anaunga mkono juu ya sarufi majumui kuwa kifaa wezeshi katika ujifunzaji wa L2. Hii ni kwa vile anaamini bado maarifa ambayo mjifunzaji wa L1 anayoyatumia katika ujifunzaji wa lugha hiyo, ndiyo yale yale anayoyatumia mjifunzaji wa L2.

Hata hivyo, Clahsen na Muysken (1986) wanasema uamiliaji wa L2 ni tofauti na uamiliaji L1 kwa vile mwuamiliaji wa L1 huwa na kifaa wezeshi cha uamiliaji lugha wakati L2 hutumia mbinu za L1 katika kujifunza L2. Wanaendelea kusema mwamiliaji wa L2 huhitaji nadharia ya isimu wakati wa ujifunzaji L2 huhitaji nadharia tambuzi.

Ellis (1996) anaeleza kuwa kifaa cha uamiliaji L1 kinaweza kutumika katika uamiliaji wa L2. Kama kanuni badilifu za L1 na ya pili zina uhusiano hurahisisha ujifunzaji. Hivyo yeye anakubali kabisa kuwa sarufi majumui ni kifaa wezeshi katika

ujifunzaji wa L2, anaamini sifa za mjifunzaji wa L1 ndizo ambazo anakuwa nazo mjifunzaji wa L2.

Aidha Ellis (1994) anaeleza ubora wa sarufi majumui kuwa imetoa msingi wa uibukaji wa nadharia zingine za ujifunzaji lugha baada ya kuegemea kwenye maarifa asilia anayozaliwa nayo binadamu. Pia imeweza kueleza sifa majumui za lugha mbalimbali za ulimwengu kwa ufupi, hivyo kusababisha sifa za lugha kueleweka kwa urahisi kwa wajifunzaji wa L2.

Kwa mujibu wa Fromkin, Rodman na Hyams (2007), ujifunzaji wa L2 kwa watu wazima hutegemea mfumo wa kisarufi wa lugha yao ya kwanza. Baadhi ya makosa yanayojitokeza wakati wahusika hao wanapojifunza L2 hujikita katika uhamishaji wa kaida za kisarufi za L1. Wanaisimu hao wanatoa mifano ya athari ya L1 ambayo ni: Kwanza, athari za kimatamshi ambapo Mjapani anayejifunza Kiingereza anashindwa kutofautisha kati ya "*write*" na "*light*" kwa kuwa [r] na [l] si fonimu katika lugha yao. Pili, anayejifunza lugha ya kigeni anaweza kushindwa kubaini tofauti kati ya konsonanti ndefu kama vile Mwiingereza anayejifunza Kiitaliano kushindwa kubaini konsonanti za aina hizo mbili ambazo hutumiwa kutofautisha maana za maneno katika lugha hiyo.

Kutokana na maelezo ya watalaam kuhusu majumui tunaona kuwa sifa za lugha huingiliana, hivyo mwingiliano wa L1 na L2 unaweza kumwezesha mjifunzaji wa L2 pale miundo ya L1 na L2 itafanana, na hata kutofautiana mjifunzaji anakuwa na uwezo wa kujiundia miundo yake itakayomsaidia katika ujifunzaji wake kwa kutumia sifa majumui za lugha.

Nchini Burundi, Kiswahili ni L2 na ni somo la lazima katika shule za sekondari, pia hufanywa kama mojawapo ya kozi katika vyuo vikuu. Humu, uamiliaji wa lugha ya Kiswahili unakabiliwa na changamoto kubwa ambazo ni athari za Kirundi (kama lugha mama).

Katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 huwa kuna baadhi ya tofauti zinazojitokeza katika viwango vya kiisimu kama fonolojia, mofolojia,sintaksia na semantiki. Tafiti nyingi zinadhihirisha maelezo hayo. Rapando (2005) alichunguza makosa ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika uandishi wa insha jijini Nairobi. Katika utafiti wake, aligundua kwamba baadhi ya makosa yanasababishwa na L2, Kiingereza na Sheng. Aidha, ujumlishaji mno ulidhihirika kusababisha makosa ya kimofosintaksia.

Corder (1981) naye anaeleza kuwa kila lugha ina muundo wake na kuhamisha sauti au mpangilio wa L1 katika L2 hudhihirika kama makosa. Hali hii ndiyo ilitupa msukumo wa kuzichunguza athari za kimofofonolojia za Kirundi kama L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2. Utafiti huu unalenga kuchunguza namna Kirundi kama L1 inavyoathiri kimofofonolojia ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2.

### 2.2.3 Athari za L1 katika L2

Robert Lado (1950), mwasisi wa athari za L1 kwenda L2 katika ujifunzaji, alianza kushughulikia kwa utaratibu makosa katika lugha, halafu akaasisi nadharia ya Uchanganuzi linganishi (*Contrastive analysis*) kwa ajili ya kuyashughulikia makosa katika lugha. Mkabala wa kinadharia wa Uchanganuzi linganishi unadai kuwa kikwazo kikubwa katika ujifunzaji wa L2 huwa ni mwathiriano wa L1 na L2.

Mkabala huu ulilenga “ulinganishi wa lugha ama mbili au zaidi ili kubainisha tofauti na ufanano baina ya lugha hizo” (Fisiak, 1981: 1).

Lado (1957 ) anaeleza juu ya matatizo yanazojitokeza katika kujifunza lugha kwa msingi wa kulinganisha kati ya L1 ya mwanafunzi na L2 anayejifunza. Katika kitabu chake *Linguistics across Cultures: Applied Linguistics for Language Teachers* anasisitiza ukweli kwamba ni kwa kulinganisha lugha mama na lugha ya kigeni kunapotokea ufunguo wa urahisi au ugumu wa kujifunza L2. Mtalaam huyu anasema kwamba kwa sababumwanafunzi huhamisha tabia za lugha mama katika kujifunza lugha ya kigeni, kuna chanzo kikuu cha ugumu au urahisi katika kujifunza lugha ya kigeni. Mtalaam huu anasema kuwa miundo ambayo itakuwa sawa na hiyo itakuwa rahisi kujifunza, kwani itahamishiwa moja kwa moja kwa lugha nyingine na itafanya kazi kwa kuridhisha ndani yake. Miundo ambayo ni tofauti nayo itakuwa ngumu kuhamisha, kwa sababu haifanyi kazi kwa kuridhisha katika lugha ya kigeni na italazimika kubadilishwa kwa njia inayofuata. Tunaweza kusema kwamba kiwango cha udhibiti wa miundo hii tofauti ni fahari si ya ujifunzaji wa lugha uliopatikana na mtu fulani.

Kama Lado anavyoeleza, kwa kuwa mwanafunzi huwa anahamisha kanuni za lugha mama, hapa tuna chanzo kikuu cha ugumu au urahisi katika kujifunza miundo ya lugha ya kigeni. Miundo hiyo ambayo ni sawa itakuwa rahisi kujifunza kwa sababu itahamishwa na inaweza kufanya kazi katika kujifunza lugha ya kigeni. Miundo ambayo ni tofauti itakuwa ngumu kwa sababu ikihamishwa haitafanya kazi kwa kuridhisha katika lugha ya kigeni na kwa hivyo italazimika kubadilishwa. Tunaweza kusema kwamba kiwango cha udhibiti wa miundo hii ambayo ni tofauti ni faharisi.

Kwa mujibu wa Lado (1957), katika ujifunzaji wa lugha kuna ugumu na vizuizi. Kiini au sababu kuu ya ugumu na kutokea kwa makosa katika ujifunzaji wa lugha ya pili inatokana na uhamishaji wa dhana kutoka L1 hadi L2. Corder (1967) anaeleza kuwa matatizo yanayojitokeza mtu anapojifunza L1 na L2 ni jambo la kawaida kutokea kabla ya mtumizi lugha kuzoea matumizi kamili ya kanuni za L2. Anaeleza kwamba, kuna tofauti kati ya makosa na matatizo. Kwake Corder, makosa ni matatizo yanayotokana na utendaji na hayana ruwaza yoyote na yanaweza kutokea kwa hali zozote. Aidha, makosa hayana uzito kama vile matatizo kwa sababu matatizo yanadhihirika kwa kuzingatia umilisi wa lugha.

Kutokana na kazi ya Selinker (1969), tunapata kuwa kuna mifanyiko mitano ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika kuchanganua athari za lugha mama katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Mifanyiko hiyo ni pamoja na ujumlishaji mno kutokana na mifumo ya L2 inayotumiwa kiholela, uhamishaji lugha ambapo kanuni za L1 hutumiwa na hivyo kukiuka kanuni za L2, mikakati ya mawasiliano katika L2, njia za kujifunza zisizokuwa halisi, na uhamishaji wa ufundishaji ambapo makosa hutokana na kutokuwa na umilisi kwa wanaofundisha. Kila aina ya tatizo hudhihirika katika njia hizo alizotaja Selinker. Kulingana na Selinker, makosa hayo yanaibua kiwango kingine katika matumizi ya lugha kinachoitwa lugha kadirifu. Lugha kadirifu ni lugha inayojitokeza wakati ambapo mzungumzaji yuko katika harakati za kujifunza L2. Mzungumzaji wa lugha kadirifu huhamisha kanuni za L1 kwa lugha lengwa.

Kazi hii ya Selinker ilichangia katika kazi yetu kwa kuwa ilituwezesha kuziainisha athari zilizoodhihirika katika kazi za kimazungumzo na kimaandishi za wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama L2 kwa kutumia baadhi ya vigezo alivyovitaja, yaani

ujumlishaji, uhamishaji wa kanuni za L1 na kukiuka kanuni za L2, na mikakati ya mawasiliano katika L2. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba Selinker alishughulikia lugha kwa jumla kwa kurejelea vipengele mbalimbali. Utafiti huu uliangazia athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi (L1) katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2).

Kwa mujibu wa Fromkin, Rodman na Hyams (2007), ujifunzaji wa L2 kwa watu wazima hutegemea mfumo wa kisarufi wa L1 yao. Baadhi ya makosa yanayojitokeza wakati wahusika hao wanapojifunza L2 hujikita katika uhamishaji wa kaida za kisarufi za L1.

Mawazo ya Nickel (1971), Lange (1974) na Corder (1973) yanakubaliana kwamba athari ya L1 kwa L2 inatokea katika nyanja zote za isimu; yaani fonolojia, mofolojia, mofofonolojia na hata sintaksia. Mawazo haya yanaungwa mkono na Valdman (1975) aliyeorodhesha data za lugha 246 zilizo na athari za L1 kwa L2 katika sintaksia, matamshi tahajia na msamiati. Kwa mujibu wa Brown (1993), athari za L1 kimatamshi kwa wanafunzi wanapojifunza L2 hutokea kwa kuwa wanafunzi hao hawatambui mfumo wa kanuni za lugha husika. Aidha, mtaalamu huyo anasema kuwa wanafunzi wengi hukosa ujuzi katika L2, kwa hivyo hawawezi kutambua athari katika lugha hiyo.Vilevile anaongezea kuwa athari katika lugha mara nyingi zina uzito na pia hudhihirika pale mwanafunzi anapotumia lugha.

### 2.2.4 Tafiti Zihusuzo Athari za Lugha Nyingine za Kibantu katika Lugha ya Kiswahili

Akichambua insha za wanafunzi kuhusiana na makosa yanayotokana na athari za lugha za Kibukusu, Were (1996) alibainisha kwamba lugha ya Kibukusu ilisababisha viwango vikubwa vya makosa yanayopatikana katika insha za wanafunzi hasa

makosa ya tahajia na msamiati. Utafiti huu ulibaini kuwa kuna hali ya wanafunzi kujumlisha sheria na kuzihamisha kutoka L1hadi L2 ambayo ni Kiswahili sanifu. Kazi ya msomi huyu ilitusaidia katika kutambua baadhi ya vyanzo vya makosa katika lugha ya Kiswahili. Utofauti mi kuwa yeye alishughulikia makosa ya kimsamiati, tahajia na sarufi ilhali tulioufanya ulihusu athari za kimofofonolojia. Were alishughulikia athari za lugha ya Kibusu kama L1 lakini utafiti tuliofanya ulishughulikia athari za lugha ya Kirundi.

Naye Otiende (2013) alichunguza athari za kimofofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili kama L2.Utafiti huu ulidhihirisha kuwepo kwa tofauti kubwa baina ya mifumo ya fonimu za Kiswahili na Kiolusuba ambao huathiri matumizi ya Kiswahili. Aidha, ameshughulikia suala la athari za Kiolusuba L1 katika matumizi yaKiswahili L2. Utafiti huu ni wa manufaa kwa kuwa ulitupa msingi wa kuelewa chanzo cha makosa yanayofanywa na wanafunzi. Utofauti ni kuwa kwanza, utafiti huu unachunguza athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi. Pili,Katika utafiti wake alitumia Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia. Mtafiti aliwashirikisha wanafunzi wa darasa la nne, sita, na nane kutoka shule za msingi ambazo zinapatikana katika kisiwa cha Mfangamano. Utafiti wa Otiende ulitofautiana na huu tuliofanya kwa kuwa, kwanza, alijishughulisha na athari ya lugha ya Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili. L1 ni Kiolusuba na L2 ni Kiswahili.

Uchanganuzi wake ulihusu kipengele cha kimofofonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kiolusuba wa darasa la nne ilhali utafiti tuliofanya ulishughukia wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi wanapojifunza Kiswahili. Pili, alishirikisha wanafunzi wa

darasa la nne, sita na nane kutoka shule za msingi za eneo la Ziwa Victoria lakini tulioufanya ulishirikisha wanafunzi wa vyuo vikuu mwaka wa kwanza nchini Burundi. Tatu, utafiti wake umetumia Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ilhali huu ulitumia Nadharia ya Uchanganuzi linganishi.

Katika utafiti wake, Nyanda (2015) alichunguza athari za Lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza Kiswahili. Utafiti wake umedhihirisha athari hizo katika nyanja za msamiati, matamshi na maana. Kwa upande wa msamiati, mtafiti aliona kuwa baadhi ya Wanyamwezi wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya kuingiza msamiati wa lugha ya Kinyamwezi katika lugha ya Kiswahili. Kwa upande wa matamshi, alibaini kwamba baadhi ya wanzungumzaji wa Kinyamwezi wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya kubadili matamshi sahihi ya sauti wakati wanapotamka neno na badala yake kutumia matamshi yasiyo sahihi. Makosa hayo si tu hufanya neno linalotamkwa kutokuwa sahihi bali pia huweza kupoteza maana ya neno lenyewe. Baadhi ya wazungumzaji wa Kinyamwezi huchopeka silabi mojawapona pia hudondosha baadhi ya sauti wakati wa ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili watoapo sentensi za Kiswahili. Kwa upande wa maana alibaini kuwa baadhi ya wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kinyamwezi wazungumzapo lugha ya Kiswahili hutafsiri maneno au sentensi zilizoko katika lugha yao na kuzitumia katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulichangia katika kazi yetu kwa sababu ulitupa mwelekeo wa kubaini makosa ya kimazungumzo ya lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wazungumzaji wa Kirundi kama L1 yao.

Naye Mashaka (2015), akichunguza athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi, aligundua kuwa athari za matamshi

zinazojitokeza kwa wanafunzi wanapojifunza lugha ya Kiswahili ni pamoja na udondoshaji wa sauti, kutumia sauti zinazokaribiana na kuongeza viambishi visivyohitajika. Aidha utafiti huo umegundua sababu zinazotokana na athari hizi ni lugha mama na athari za kimazingira. Utafiti huo ulichangia katika utafiti huu kwa kuwa ulimfafanulia athari za kimatamshi zinazodhihirika kwa wanafunzi wa Kiswahili. Hata hivyo, kazi ya Mashaka ilitofautiana na hii kutokana na hali kuwa, mtafiti huyu alijikita na lugha ya Kijita ilhali katika kazi hii mtafiti alichunguza athari za mofofonolojia ya Kirundi kwa lugha ya Kiswahili, lugha za kibantu lakini tofauti.

Akishughulikia masuala ya kiisimu katika ufundishaji wa lugha, Wilkins (1972) anasema kwamba makosa ya matamshi, tahajia, sarufi, na msamiati yana mtindo wa kujitokeza katika lugha za wahusika mbalimbali. Hivyo, kutokana na ushahidi wa kasoro au dosari za lugha, pana uwezekano wa kuainisha athari za lugha L1 katika L2. Kutokana na hali hii, alishauri kwamba mazungumzo na maandishi ya mwanafunzi anayejifunza lugha ya kigeni yakichunguzwa, hapana shaka kwamba baadhi ya kasoro zina chanzo chake katika L1. Alielezea zaidi kuwa katika jitihada za mwanafunzi kufanya matamshi ya lugha ya kigeni anaathiriwa na sauti zilizomo katika mfumo wa L1, idadi yake, na hali za kifonolojia za sauti hizo.

Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kwamba tofauti za mfumo sauti wa Kiswahili na ule wa Kitigania ni chanzo kikubwa cha athari za kifonolojia na kimofolojia. Alifafanua kwamba, kadri ambavyo tofauti kati ya lugha zinavyozidi, ndivyo ambavyo vikwazo vya kujifunza L2 vinavyoongezeka. Utafiti huu ulimpa mtafiti msingi wa kuelewa chanzo cha makosa yanayofanywa na wanafunzi.

Akishughulikia suala la kuathiriana kwa Kiswahili na lahaja ya Kitigania, Mukuthuria (2004) alibaini ya kwamba kuna matatizo mengi ya kiisimu yanayowakumba wanafunzi wanaotumia lugha ya Kitigania wanapojifunza Kiswahili. Matatizo anayoyataja ni pamoja na yale ya kitahajia, kisarufi, uchanganyaji ndimi na kutafsiri dhana za Kiswahili kwa misingi ya Kitigania. Uchunguzi uliofanywa na mwanataaluma huyo ulithibitisha kwamba, chanzo cha matatizo hayo ni mifumo ya kifonolojia na kimofolojia ya lugha hizi.

Akishughulikia suala la kuathiriana kwa Kiswahili na Kigisu nchini Uganda, Haroon (1998), aligundua kuwa Kigisu kiliathiri mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiswahili. Anasema kuwa, kutokana na tofauti za kimuundo kati ya lugha hizi mbili, watafitiwa walihamisha muundo wa nje wa kisintaksia wa Kigisu (L1) kwa Kiswahili (L2). Hali hii ilikuwa chanzo cha makosa aliyogundua Haroon katika mpangilio wa maneno katika sentensi zilizotungwa na watafitiwa husika. Utafiti huu ulitufaidi kwa kuwa ulimfafanulia mtafiti baadhi ya vyanzo vya makosa katika matini za wanafunzi wa shule za upili. Hata hivyo, kazi ya Haroon ilitofautiana na kazi hii kutokana na hali kuwa alijikita katika kipengele cha sintaksia ilhali utafiti huu ulizamia katika kipengele cha athari za mofofonolojia.

Akishughulikia kuibuka kwa ‘Viswahili’ ndani ya Kiswahili, Munyua (2002) anasema kuwa athari za L1 kwa L2 husababisha makosa mbalimbali ya kimatumizi. Anaitumia dhana ya ‘Viswahili’ kurejelea matumizi potofu ya lugha ya Kiswahili kutokana na uhamishaji hasi kutoka kwa lugha mbalimbali za kwanza kama vile: Kibukusu, Kikisii, Kikikuyu, Kimeru, Kikalenjin na Kiluo. Alisisitiza kuwa athari husika hujitokeza katika viwango vyote vya lugha ambavyo ni: fonolojia, mofolojia,

sintaksia na semantiki. Kuhusu idadi ya makosa katika matamshi, Munyua alishikilia kuwa iwapo makosa ni mengi, tamko husika hukanganya; hivyo kutokueleweka. Alipendekeza kuwa tafiti zifanywe kuhusu 'Viswahili' kwa lengo la kuwaelekeza watunga mitaala ya Kiswahili kutafuta mbinu mpya za ufundishaji wa Kiswahili sanifu.

Kwa mujibu wa Ngugi (2007), L1 huathiri ujifunzaji wa L2 katika kiwango cha fonolojia. Katika kuchunguza namna lugha ya Kikikuyu ilivyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, mtafiti huyu aligundua kuwa athari husika zilijitokeza katika matamshi na pia katika tahajia. Ngugi amesisitiza kwamba makosa mengi yaliyojitokeza katika matumizi ya lugha ya wanafunzi wa shule za upili waliotumiwa kama watafitiwa, yalitokana na uchopekaji, udondoshaji na unazalishaji. Ameeleza kwamba, mifanyiko hiyo ya kifonolojia ilidhihirika katika matumizi ya lugha ya wanafunzi husika huku makosa yakijitokeza kutokana na tofauti katika mifumo ya lugha hizi mbili.

Akichunguza athari ya lugha ya Kimakonde katika kujifunza lugha ya Kiswahili, Mpangala (2018) alibainisha matatizo ambayo watoto wa Kimakonde wa shule za msingi wanakutana nayo wanapokuwa wanajifunza lugha ya kiswahili. Uchunguzi huu ulichochewa na kuwepo kwa makosa ya matumizi ya Kimakonde (L1) katika lugha ya Kiswahili (L2), makosa hayo ni ya kimatamshi, msamiati, maana na matatizo ya kisarufi. Kazi hii ya utafiti ilimfaidisha mtafiti kwa kuwa ilimwonyesha mtafiti makosa yanayatokana na L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2.

Naye Joyce (2019), akichunguza athari za lugha ya Kinyaturu katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2, aliona kuwa athari za lugha ya Kinyaturu katika ujifunzaji wa

Kiswahili ziko kwenye semantiki (kimaana), msamiati, na matamshi. Kwa mujibu wa utafiti huo, zipo sababu zinazosababisha kutokea kwa athari za lugha ya Kinyaturu katika kujifunza lugha ya Kiswahili kama vile ufundishaji mbaya wa somo la Kiswahili, lugha ya Kiswahili kutopewa kipaumbele, kudumisha utamaduni wa Kinyaturu, mazingira duni ya kujifunza lugha ya Kiswahili, na lugha ya Kinyaturu kutumika kama utambulisho. Mtafiti aliweza kubaini mbinu ambazo zinaweza kutumika katika kuwasaidia wanafunzi walioathirika kwa L1 wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Mbinu hizo ni watoto wafundishwe lugha ya Kiswahili tangu utotoni, walimu wawe mahiri katika kufundisha Kiswahili, kuwe na mazingira rafiki ya kujifunza Kiswahili, na wazazi au walezi wa watoto wahamasishwe kutumia Kiswahili. Utafiti huu ulimfaidisha mtafiti kwa kuwa ulimpa mwangaza juu ya makosa ya kimatamshi yanayotokana na athari za lugha mama. Hata hivyo, kazi ya Joyce ilitofautiana na utafiti huu kwa kuwa katika kazi yake alijikita katika athari za Kinyaturu katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa ujumla ilhali utafiti huu ulijikita katika kipengele cha athari za kimofofonolojia ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili.

### 2.2.5 Kazi Mahususi Zinazohusu Athari za Lugha ya Kirundi kwenye L2

Katika utafiti wake, Bamporubusa (2012) alichunguza matatizo yanayojitokeza katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika ngazi ya pili ya shule ya msingi nchini Burundi. Mtafiti huyu aliona kwamba athari za lugha ya Kirundi katika Kiswahili zinasababisha baadhi ya makosa ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Makosa hayo yanajitokeza katika mazungumzo na maandishi ya Kiswahili. Utafiti huu ulitufaidisha kwa kuwa aligusia makosa yote yanayotokana na athari za Kirundi katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, utafiti huo ni tofauti na utafiti wetu kwa sababu utafiti huo uliegemea kwa matatizo katika

ufundishaji wa Kiswahili lakini kazi hii iliegemea katika athari za kimofofonolojia zalugha ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa vyuo vikuu wa jamiilugha ya Kirundi.

Ntawiyanga (2015) kwa upande wake alichunguza makosa ya upatanishi wa kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa makosa yanayofanywa na wanafunzi Wanyarwanda yanatokana na athari za L1 yao wanapotaka kujumuisha kanuni za lugha ya Kiswahili.

Naye Niyonizeye (2013), akichunguza changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu nchini Burundi, alibainisha makosa mbalimbali ambayo wanafunzi Warundi wajifunzao Kiswahili hufanya wanapozungumza. Utafiti huo unatoa mchango kwa utafiti huu kwa upande wa makosa ya kimatamshi ya Kiswahili yanayotokana na Kirundi kwa kuwa kazi hii inachunguza athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili.

Akichunguza makosa yanayojitokeza katika vitabu vya Kiswahili vya shule za msingi nchini Burundi, Niyubahwe (2017) alibaini na kuorodhesha makosa kwenye vitabu vya wanafunzi na walimu. Aligundua pia kuwa makosa hayo yalitokana na uhaba wa ujuzi wa watunga mitaala ya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili sanifu.

Naye Mbonabuca (2019) anaeleza kwamba lugha ya Kinyarwanda inaathiri sana lugha ya Kirundi. Warundi wengi wanaoishi nchini Rwanda, haswa wa mijini na wanafunzi, wanaathiriwa sana na Kinyarwanda. Lugha wanayoitumia inaweza kuwa pijini ya lugha ya Kibantu kati ya Kirundi na Kinyarwanda.Utafiti huo unachangia

katika kazi hii kwa kuonyesha jinsi lugha zenye miundo inayokaribiana kufanana zinaathiriana.

Alipochunguza matumizi ya lugha ya Kiingereza, mitazamo ya wanafunzi kuihusu na athari zake kwa Kirundi na Kifaransa, Irakoze (2015) aligundua kuwa lugha ya Kiingereza imeanza kuathiri matumizi ya lugha nchini Burundi. Zaidi ya hayo, Kiingereza kinathaminiwa sana na wanafunzi wa Burundi kuwa lango la maendeleo yanayotamaniwa zaidi ya Kifaransa na Kirundi ambayo inaweza kufanya au imeshindwa kufanya. Utafiti huo unachangia kwa kuonyesha jinsi swala la athari linajitokeza pale ambapo lugha mbili tofauti au zaidi zinapozungumzwa.

Mawazo ya wataalamu hawa wote yanaonesha kuwa katika ujifunzaji wa L2 imejitokeza wazi kuwa L1 huathiri L2 hususani zile na kusababisha makosa ya aina mbalimbali. Ni kutokana na msingi wa mawazo ya wataalamu hawa utafiti huu ulichunguza namna lugha ya Kirundi inavyoathiri mofofonolojia ya Kiswahili kama L2 katika ujifunzaji wake.

## 2.3 Pengo la Utafiti

Kutokana na mapitio hayo mbalimbali, mtafiti ameona kwamba tafiti nyingi zimefanyika juu ya makosa na athari za lugha mama katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha L2. Ingawa kumekuwa na juhudi za kuimarisha na kuboresha lugha ya Kiswahili kama L2, tafiti nyingi zinaonyesha kwamba wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili hufanya makosa katika mazungumzo na mandishi yao. Baadhi ya makosa hayo ni pamoja na makosa ya kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki, kifonolojia na kimofofonolojia. Hata hivyo, kati ya tafiti hizo kutokana na uelewa wetu hakuna tafiti zilizoelezea kuhusu athari za mofofonolojia

ya Kirundi katika kujifunza Kiswahili kama L2 katika vyuo vikuu nchini Burundi. Hivyo utafiti huu utajikita katika kutathmini athari za mofofonolojia ya Kirundi kama L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2kwa kubaini aina za athari hizo, kutathmini viwango vya utamalaki wa aina mbalimbali za athari hizo na kubainisha mbinu za walimu kubaini na kukabiliana na athari za kimofofonolojia za Kirundi kama L1 ya wanafunzi.wajifunzao Kiswahili kama L2 ili kuziba pengo hili la maarifa.

## 2.4 Kiunzi cha Nadharia

Ili utafiti ufanyike kwa uaminifu na uthabiti wenye kuzaa matunda tarajiwa kulingana na malengo ya utafiti huo, ni lazima uongozwe na nadharia sahihi kwani nadharia hiyo hubeba mawazo, dhana au maelezo yatolewayo kwa nia au kwa lengo la kueleza hali fulani, chanzo, muundo au utendaji wa jambo.

Kuna mitazamo mbalimbali inayotumika kueleza jinsi mwanafunzi anavyojifunzaL2. Mitazamo hii ni kama vile Uchanganuzi Linganishi na Uchanganuzi Makosa. Utafiti huu utaongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Linganishi.

### 2.4.1 Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi

Kwa mujibu wa Stern (1983), Nadharia ya Uchanganuzi-linganishi iliasisiwa miaka ya 1950 kama mbinu ya ufunzaji wa lugha iliyokuwa na misingi yake katika isimu miundo. Awali, ilitumika kulinganisha lugha mbili katika hatua zake za kimaendeleo. Aidha, ilitumika kulinganisha lugha mbili au zaidi katika vima mbalimbali ili kubainisha tofauti na ulinganifu wa lugha hizi. Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Fries, Weinrich, Haugen na Lado. Kwa mujibu wa Stern (1983), kazi ya Lado (1957) ilikuwa kazi ya mwanzo kabisa kuanzisha matumizi ya kisasa ya nadharia hii.

Inashikilia kuwa mifumo miwili ya lugha inaweza kulinganishwa, na matokeo ya ulinganisho huu yakatumiwa na waalimu wa lugha kuimarisha ufundishaji wa L2. Utaratibu unaofuatwa katika kuchanganua vipashio vya lugha ni kuvilinganisha na kuvitofautisha ili kudhihirisha jinsi vinavyofanana na kutofautiana. Kwa mujibu wa nadharia hii, kufanana baina ya lugha mbili kunarahisisha ujifunzaji wa L2, na kutofautiana baina ya lugha hizo kunatatiza ujifunzaji wa lugha lengwa (Lado, 1957). Ni katika mwelekeo huu ambapo ilidhihirika kwamba, uchanganuzi-linganuzi ukifanyiwa lugha ya Kirundi (L1) na lugha ya Kiswahili (L2), matokeo ya utafiti huu juu ya athari za kimofofonolijia za lugha ya Kirundi katika kujifunza Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi, yanaweza kueleweka kwa undani, na hivyo, yakaimarisha ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Burundi. Nadharia hii ilipata uimara zaidi kutokana na kazi ya James (1980) katika kitabu chake *Contrastive Analysis.* Katika kazi hii, msomi huyu amedhihirisha jinsi nadharia hii inavyoweza kuchanganua lugha katika vipashio mbalimbali kama vile, fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Pia, anapendekeza kuwa wanaisimu hawana budi kujaribia nadharia hii katika vipashio vikubwa kuliko sintaksia kama vile matini.

### 2.4.2 Hatua za Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi

James (hapo juu) akifafanua jinsi Uchanganuzi-linganuzi unavyopaswa kutekelezwa, anawaadhi kuwa hatua mbili zinapaswa kuzingatiwa: Kwanza, ni kutoa maelezo kwa lugha zinazohusika katika vima vinavyochanganuliwa; pili, kulinganisha maelezo ya L1 na L2.

### 2.4.3 Sababu za Kuchagua Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi

Nadharia hii imeteuliwa kwa sababu ; kwanza Nadharia hii ina uwezo wa kuelezea kiini cha wanafunzi kufanya makosa wanapojifunza L2. Sababu ya pili ni kuwa nadharia hii ina uwezo wa kuonyesha uwiano na tofauti kati ya lugha mbili. Sababu ya tatu ni kutokana na utaratibu wa kulinganisha na kulinganua, na vipengele vinavyoweza kutatiza ujifunzaji wa lugha lengwa vinaweza kubainika. Habari hiyo inaweza kumfaidi mwalimu na mwanafunzi wakati wa kufunza na kujifunza lugha.

Kwa jumla nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ina manufaa ya moja kwa moja.

Kutokana na maelezo hayo yote, nadharia ya Uchanganuzi Linganishi imebainika kuwa ni mwafaka kwa utafiti huu. Nadharia hii imeundwa kwa lengo la kuchunguza athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi L1 zinazowakumba wanafunzi wa vyuo vikuu wanapojifunza Kiswahili kama L2 nchini Burundi.

## 2.5 Hitimisho la Sura ya Pili

Katika sura hii kumeshughulikiwa mapitio ya maandiko na tafiti tangulizi kuhusu dhana ya mofofonolojia, sarufi majumui na uamiliaji, athari za L1 katika ujifunzaji wa L2, athari za lugha nyingine za kibantu katika lugha ya Kiswahili na kazi mahususi zinazohusu athari za lugha ya Kirundi kwenye L2. Pia, kumejadiliwa pengo la utafiti na kiunzi cha nadharia iliyoongoza utafiti huu. Sura inayofuata inashughulikia watafitiwa na mbinu mbalimbali za kukusanya data.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sehemu hii inaelezea usanifu wa utafiti, mkabala wa uchambuzi wa data, eneo la utafiti, sampuli, usampulishaji, mbinu za utafiti na maadili ya utafiti. Ili kufikia malengo ya utafiti kwa njia mwafaka katika mipaka ya nadharia husika, mbinu za utafiti lazima ziainishwe.

## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni kama ramani inayotanabaisha sura nzima ya utafiti inavyopaswa kuwa tangu katika ukusanyaji wa data mpaka uandishi wa tasinifu nzima (Kothari, 2008; Babie, 1999). Usanifu wa utafiti unatoa fursa ya kuchunguza jambo kwa undani zaidi na kuhusisha vipengele muhimu vilivyojenga kazi ili kupata majibu ya utafiti (Isaac na Michael, 1981). Lakini pia Yin (1994) na Robson (2007) wanasema mbinu hii inasaidia kutoa majibu ya maswali kama vile : kwa nini ? kwa sababu gani ? Kwa mantiki hiyo, mbinu hii itaweza kujibu maswali ya utafiti yanayolenga kuchunguza athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi katika uamiliaji wa Kiswahili kama L2.

Kuna aina mbalimbali za usanifu wa utafiti baadhi yake ni usanifu wa kidhahania, usanifu wa kuchunguza kwa makini, usanifu wa kimaelezo, usanifu wa kidata na usanifu wa uganini. Lakini katika utafiti huu, mtafiti alitumia uchunguzi wa kimaelezo na kitakwimu. Usanifu wa maelezo kama ulivyofafanuliwa na Cohen (2007) ni kupanga, kutoa sababu na kuzielezea data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti. Mtafiti huzipanga taarifa kutokana na maudhui au makundi yanayofanana.

Mtafiti alikuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki, kuvumbua, kutafsiri taarifa alizozipata kupitia muundo huu wa utafiti. Hata hivyo, utafiti huu umetumia takwimu kama kielelezo.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Kabla ya kukusanya data za utafiti ni muhimu kuchagua mahali ambapo upatikanaji wa data utatosheleza majibu ya maswali ya utafiti, na hivyo kufanikisha lengo la utafiti. Ngure (2011) anaeleza kwamba inabidi kuamua ni wapi utakusanya data unazohitaji.

Utafiti huu ulifanyika jijini Bujumbura katika Vyuo Vikuu vitatu: Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu (Université des gands Lacs, UGL), Chuo Kikuu cha Busara ya Afrika (Université Sagesse d'Afrique, USA) na Chuo Kikuu cha Mwaro (Université de Mwaro, UM). Watafitiwa walikuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza (Bac1) na walimu wa Kiswahili katika vyuo vikuu. Uteuzi huu ulitokana na kuwa vyuo hivi vina vitivo vinavyoandaa ufundishaji wa somo la kiswahili kwa muda wa masaa mengi ukivilinganisha na vitivo vya ufundi.

### 3.4 Sampuli

Babbie (1992) anasema kwamba, sampuli ni sehemu ya idadi ya watu ambayo mtafiti anavutiwa nayo katika kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake. Sampuli ni istilahi inayotumiwa katika masuala ya utafiti kurejelea wahojiwa wachache kutoka kundi lengwa ambalo huteuliwa na mtafiti ili watumike kutoa taarifa zinazochunguzwa na mtafiti (Kothari, 2004). Kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti. Kothari (2004); Bryman (2004); Kombo na Tromp (2006). Katika utafiti huu mtafiti alitumia sampuli za wanafunzi wa Vyuo Vikuu

vitatu ambao ni wazungumzaji wa Kirundi na walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika vyuo. Uteuzi wa vyuo na madarasa tafitiwa ulijikita kwenye ufundishaji wa Kiswahili kama kozi muhimu ya lazima. Sampuli zilisakwa nyanjani kutoka Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu (Université des gands Lacs, UGL), Chuo Kikuu cha Busara ya Afrika (Université Sagesse d'Afrique, USA) mjini Bujumbura na Chuo Kikuu cha Mwaro (Université de Mwaro, UM) mkoani Mwaro (kijijini). Watafitiwa walikuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza (Bac1) kwa upande mmoja, kwa upande mwingine ni walimu wa Kiswahili katika chuo. Kwa hivyo, mtafiti alifanya uchunguzi wa athari za kimofofonolojia za Kirundi kama L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2.

Kiutafiti, sampuli ya wahojiwa hutakiwa ijitosheleze na iwe inayotokana na kile mtafiti anachotaka kukitafiti ambapo sampuli hiyo itakuwa inawakilisha eneo msingi la utafiti. Kwa hiyo, kutokana na maelezo ya hapo juu, sampuli ya utafiti huu ilihusisha wahojiwa wanafunzi 100 na walimu 8. Mtafiti aliamua kutumia idadi hii ya wahojiwa kutokana na ukweli kwamba si jambo rahisi kutafiti kundi kubwa la watu. Hivyo, ili kukamilisha utafiti huu kwa wakati, mtafiti aliamua kutumia sampuli ya watu wachache. Hata hivyo idadi hii ya wahojiwa wanafunzi 100 na walimu 8 kama ilivyo kwenye Jedwali namba 3.1 inatosheleza kutoa taarifa zinazotakiwa kwa utafiti huu.

Mchanganuo wa watafitiwa hao ni kama unavyooneshwa katika jedwali lifuatalo: Mgawanyo wa watafitiwa kwa kigezo cha makundi na maeneo wanayotoka ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali na.3.1.

**Jedwali Na.3.1: Mgawanyo wa watafitiwa kwa kigezo cha makundi na maeneo wanayotoka**

| **Chuo cha** | **Wanafunzi** | **Walimu** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Maziwa Makuu (Grands Lacs | 40 | 4 | 42 |
| Busara ya Afrika Sagesse d'Afrique | 40 | 3 | 42 |
| Mwaro | 20 | 1 | 21 |
| Jumla | 100 | 8 | 108 |

### 3.5 Usampulishaji

Sigh (2007) anaeleza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Kwa mujibu wa Kothari (2004), usampulishaji ni mchakato wa kuteua sampuli yawahojiwa wachache kutoka katika sampuli kuu zitakazotumika katika utafiti kuwakilisha kundi zima.

Watafitiwa wanafunzi 100 walichaguliwa kwa kutumia usampulishaji nasibu. Idadi ya wanafunzi watafitiwa ilisampulishwa kwa kwa kigezo cha 20% cha wanafunzi darasa kwa darasa na chuo kwa chuo. Katika Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu (Université des gands Lacs, UGL) na Chuo Kikuu cha Busara ya Afrika (Université Sagesse d’Afrique, USA), tulikuwa na watafitiwa 40 miongoni mwa wanafunzi 200; na katika Chuo Kikuu cha Mwaro (Université de Mwaro, UM) kulikuwa na watafitiwa 20 miongoni mwa wanafunzi 100. Pia watafitiwa 8 walikuwa walimu wa Kiswahili katika vyuo vikuu ambao waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji usio nasibu.

Kwa watafitiwa wanafunzi, kazi hii ilifanyika kwa njia mbili, njia ya maandishi na njia ya mazungumzo. Katika maandishi, darasa zima lilishirikishwa. Tuliwapa

wanafunzi hojaji na shughuli ya kuandika insha yenye mada: “Mvua iliyonyesha sana wakati huu wa masika". Kazi zao tulizipatia nambari 1 hadi 4 kwa kufululiza hadi kazi zote darasa kwa darasa zima linalokamilika na chuo kwa chuo. Hatimaye tuliziweka kazi hizo kwa makundi kulingana na mfululizo wa nambari 1 hadi 4 tulizoandika kwenye karatasi ya kazi ya kila mwanafunzi. Kisha tuliteua kundi lenye nambari 2 kuwa sampuli yetu. Tulitumia utaratibu kama huu katika madarasa yote ili kujipatia sampuli ya wanafunzi 40 katika kila chuo miongoni mwa Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu (Université des gands Lacs, UGL) na Chuo Kikuu cha Busara ya Afrika (Université Sagesse d’Afrique, USA), pamoja na sampuli ya wanafunzi 20 wa Chuo Kikuu cha Mwaro (Université de Mwaro, UM). Hatimaye hojaji na insha zilizoandikwa na wanafunzi zilikaguliwa na mtafiti na kubaini athari za kimofofonolojia za Kirundi L1 kimaandishi katika Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili. Baada ya kukagua, kubainisha na kuchanganua, mtafiti alitathmini athari za kimofofonolojia ya Kirundi zinazoibuka katika kazi za wanafunzi hao na kisha kueleza vyanzo vyake kutegemea mikakati tambuzi ya kiisimu-nafsia.

### 3.6 Mbinu za Utafiti

Kama anavyosema Kothari (2004), mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa na mtafiti katika kuufanyia kazi utafiti wake. Ziko aina kuu mbili za mbinu za utafiti, yaani mbinu za kukusanyia data na mbinu za kuchanganua data. “Mbinu za kukusanyia data ni mbinu ambazo mtafiti huzitumia ili kupata data za utafiti” (Pandu, 2017:23), ilhali mbinu za kuchanganua data ni njia au michakato ya kufasiri na kutathmini data zilizokusanywa.

### 3.6.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Hizi ni mbinu au njia zilizotumiwa na mtafiti katika zoezi la ukusanyaji wa data. Kothari (ameishatajwa) anasema kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji data. Msaghaa (2010) anasisitiza kuwa njia au mbinu za utafiti zinatoa aina za taarifa zinazohitajika kujibu swali la utafiti. Kuna mbinu kadha wa kadha ambazo hutumiwa na watafiti katika ukusanyaji wa data. Katika utafiti huu tulitumia mbinu za hojaji, ushuhudiaji na jaribio la umilisi.

#### 3.6.1.1 Hojaji

Mtafiti alitumia mbinu ya hojaji kuweza kupata taarifa alizokuwa amekusudia kuzipata katika utafiti wake. Kwa mujibu wa Kothari (2012), mbinu ya hojaji ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti anaandaa maswali yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Mbinu hii ni ya kutumia maswali yaliyoandikwa kwa lengo la kujibiwa na mtafitiwa. Aidha, Mligo (2012) anaendelea kudai kwamba, hojaji ni karatasi iliyoandikwa maswali ambayo hupewa mtafitiwa ili aandike majibu kulingana na maelezo ya wataalam hao. Hivyo, hojaji zenye maswali funge na wazi zilitumika kwa wanafunzi kukusanya data za makosa ya kimaandishi ya mofofonolojia. Hojaji kwa walimu zilitumika kukusanya data zinazohusu mbinu zinazotumiwa na walimu kukabiliana na athari za mofofonolojia ya Kirundi (L1) katika kuamilia Kiswahili (L2).

#### 3.6.1.2 Jaribio la Umilisi

Mbinu ya jaribio la umilisi ilikuwa ni kubaini na kuchanganua athari za kimofofonolojia katika maandishi ya wanafunzi waliotafitiwa. Mbinu hii ilisaidia

katika kutathmini aina za athari za kimofofonolojia kimaandishi ya Kiswahili kama L2 kwa watafitiwa kwa ajili ya lengo la kutathmini athari za kimofofonolojia za Kirundi za kimaandishi ya lugha ya Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1).

#### 3.6.1.3 Ushuhudiaji

Kama wanavyosema Buliba na wenzake (2014:96), "hii ni ratiba au mpango wa mambo au matukio ambayo mtafiti ananunia kuyatazama." Hii ina maana kuwa, mtafiti mwenyewe anapaswa kushuhudia mambo fulani kuhusiana na utafiti wake. Katika mbinu hii, inawezekana mtafiti akawatazama watafitiwa akiwa anajulikana na kushiriki apendavyo tendo la watafitiwa, au asijulikane. Katika utafiti huu, mbinu hii ilitumiwa na mtafiti katika upataji wa data za kimazungumzo. Mtafiti aliingia darasani na kugawa wanafunzi katika makundi ili waigize salamu za Kiswahili walizojifunza.Maigizo hayo yalinakiliwa katika vinasa sauti. Baadaye mtafiti alichanganua data hizo kwa ajili ya lengo la kutathmini athari mbalimbali za kimofofonolojia kimatamshi ya Kiswahili kama L2 kwa watafitiwa.

## 3.7 Mkabala wa Uchambuzi wa Data

Data zilizokusanywa zilitolewa maelezo, zilichambuliwa na kufupishwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na wa kiidadi. Kothari (2004) anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni njia ya kuchambua data katika muundo wa maelezo pasipokufuata taratibu za kitakwimu.

Kutokana na data zilizohusika katika utafiti huu ambazo uchanganuzi wake ulilenga kuchunguza athari za kimofofonolojia za Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa kutathmini, kuziainisha na kubainisha juhudi za walimu za kubaini na kukabiliana na

athari hizo, kulihusishwa mchanganyiko wa mikabala ya kimaelezo na kitakwimu. Upande mmoja, mkabala wa kimaelezo ulihusika kwa sababu ya tukio la data za kiuthamano katika utafiti huu. Upande mwingine, mkabala wa kitakwimu ulihusika na data za kiwingidadi kwa sababu utafiti huu ulihusu uchambuzi wa vipashio au viambajengo vya lugha ya Kiswahili kutokana na malengo ya utafiti huu. Aidha, jedwali lilitumika na hivyo data hizo zilifupishwa kwa namna ambayo ni rahisi kuchambuliwa na kueleweka kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu.Kulitumiwa majedwali kuwasilisha lugha kadirifu kimaandishi na kimatamshi kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine, kulitolewa maumbo sahihi ya Kiswahili sanifu kimaandishi na kimatamshi (kifonetiki)

## 3.8 Maadili ya Utafiti

Enon (1998) anasema kuwa mkabala wa maadili ya utafiti ni moja wapo ya masuala muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, akitekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake. Miongoni mwa mambo muhimu ambayo mtafiti alitakiwa kuyazingatia ni suala la maadili. Katika utafiti huu, mtafiti alizingatia maadili yaliyotakiwa kufuatwa na kuzingatiwa kama vile kupata kibali cha kufanya utafiti, kutunza siri za watafitiwa, kuheshimu mipaka ya utafiti kabla na baada ya kukusanya data. Katika utafiti huu  mtafiti alizingatia maadili hayo na kufanikisha kuyafikia malengo ya utafiti huu kwa ufanisi mkubwa.

## 3.9 Hitimisho la Sura ya Tatu

Katika sehemu hii, kumeelezwa jinsi mtafiti alivyofikia malengo ya utafiti huu kupitia njia na mbinu za utafiti. Kumeelezwa kuhusu kazi hii kwa kurejelea mambo mbalimbali kama vile  usanifu wa utafiti, eneo la utafiti sampuli, usampulishaji,

mkabala wa utafiti, uteuzi wa walengwa. Pia, kumeshughulikiwa mbinu za ukusanyaji data, mkabala wa uchambuzi wa data na maadili ya utafiti. Sura inayofuata ilijikita katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data zilizopatikana kutokana na mbinu za utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusika na uwasilishaji, uchambuzi na mjadala ya data kuhusu athari za kimofofonolojia zinazodhihirika kimatamshi na kimaandishi kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi wanaojifunza Kiswahili kama L2. Pia, uchambuzi huu uliangazia mbinu za kutumia ili kuwasaidia wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama L2. Mwisho wa sura ni hitimisho la kutamatisha mjadala uliokuwa umefanyika katika sura hii.

## 4.2 Uwasilishaji wa Data

Mtafiti alikusanya data zilizotoa taarifa kutoka uwandani. Ukusanyaji wa data ulifanyika kwa njia ya hojaji, ushuhudiaji na jaribio la umilisi. Idadi ya wanafunzi waliolengwa na utafiti huu walikuwa mia moja (100) kutoka vyuo vikuu vitatu yaani wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu , wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha Busara ya Afrika na wanafunzi 20 kutoka Chuo Kikuu cha Mwaro. Mbinu ya hojaji ilitumiwa na mtafiti kwa njia ya maswali funge na wazi ili kushadidia matokeo ya njia ya upitiaji wa nyaraka. Watafitiwa walikuwa wanafunzi kwa upande mmoja na walimu 8 wa Kiswahili katika vyuo vikuu kwa upande mwingine. Mbinu ya ushuhudiaji ilitumiwa na mtafiti kwa kugawa wanafunzi katika makundi ili waigize.Baadaye mtafiti alichambua data hizo kwa njia ya kusikiliza mara nne kundi kwa kundi, kwa ajili ya lengo la kubaini athari za kimofofonolojiaza Kirundi katika uzungumzaji wa Kiswahili kama L2 kwa watafitiwa. Mbinu ya jaribio la umilisi ilitumiwa na mtafiti katika upataji wa data za kimazungumzo na kimaandishi. Mtafiti aliwapa wanafunzi zoezi la kuandika insha yenye mada “Mvua iliyonyesha sana

wakati huu wa masika". Mtafiti alisoma kwa makini nyaraka hizo ili kubaini na kuchanganua athari za kimofofonolojia katika maandishi ya wanafunzi waliotafitiwa. Uchanganuzi wa data za utafiti huu ulijikita kwa lengo kuu la kutathmini athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2) kwa wanafumzi wa jamiilugha ya Kirundi.

## 4.3 Athari za Kimofofonolojia za Kirundi (L1) Katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili (L2)

Katika sehemu hii, mtafiti aliangazia athari za kimofofonolojia za Kirundi zinazodhihirika kimatamshi na kimaandishi kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi wanaojifunza Kiswahili (L2). Mtafiti alishughulikia malengo ya kwanza na pili ya utafiti huu. Lengo la kwanza ni kubainisha athari za kimofofonolojia za Kirundi katika Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1) na lengo la pili ni kutathmini viwango vya utamalaki wa aina mbalimbali za athariza kimofofonolojia za lugha ya Kirundi katika Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1). Katika kazi ya uchambuzi wa data, mtafiti aliainisha athari zilizotokea na kutathmini viwango vya utamalaki wake akitumia nadharia ya uchanganuzi linganishi. Michakato ya kimofofonolojia ambayo imeweza kubainika ni uchopekaji, udondoshaji na ubadala wa fonimu.

Hili linadhihirishwa kwa kina kama ifuatavyo : Uchambuzi wa data ulidhihirisha jumla ya athari 1018 ziliyogawanyika katika makundi makuu matatu, yaani athari za uchopekaji zilizojitokeza kwa kiasi cha 405, sawa na 39.78%, athari zaa udondoshaji kwa kiasi cha 102, sawa na 10.01%, na athari za matumizi ya sauti mbadala kwa kiasi cha 511, sawa na 50.19%.

Jedwali Na. 4.1 linaonesha aina hizo za athari zilizodhihirika katika utafiti huu na idadi yake.

**Jedwali Na. 4.1 : Jumla ya Aina za Athari**

| **Na.** | **Michakato ya kimofofonolojia** | **Idadi ya matokeo ya michakato** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| 1 | Uchopekaji | 405 | 39.78 |
| 2 | Udondoshaji | 102 | 10.02 |
| 3 | Matumizi ya sauti mbadala | 511 | 50.20 |
| | **Jumla ya makosa** | **1018** | **100.00** |

Jedwali Na. 4.1 linadhihirisha ujumla ya aina ya makosa yaliyojitokeza baada ya kazi ya mtafiti ya kuchanganua data za kimazungumzo na kimaandishi watafiwa wanafunzi wa Kiswahili (L2) wanaozungumza Kirundi (L1). Kwa ujumla, athari kutokana na matumizi ya sauti mbadala zilichukua nafasi kubwa, zikifuatwa na athari zinazotokana na uchopekaji na athari zinazotokana na udondoshaji zilijitokeza kwa kiasi kidogo kuliko mengine yote. Katika kila aina miongoni mwa aina hizi kuu, kuna aina ndogondogo za michakato ya kimofofonolojia kama zilivyochanganuliwa hapa chini.

### 4.3.1 Uchopekaji

Uchopekaji ni mchakato wa kimofofonolojia unaorejelea hali ambapo kipashio huongezwa katika neno. Matokeo ya hali hii ni kupatikana kwa neno ambalo linasheheni sauti ya ziada ambayo haikuwapo katika neno la msingi. Kutokana na uchanganuzi wa data ya wanafunzi wa Kiswahili (L2) wazungumzaji wa Kirundi (L1), athari za kimofofonolojia zinazotokana na uchopekaji zilidhihirika kwa kiasi cha 405 na uchopekaji uliojitokeza ulihusu irabu /u/ kwa kiasi cha 94, sawa na 23.20% , irabu /i/ kwa kiasi cha 101, sawa na 24.93% , konsonanti /h/ kwa kiasi cha

73, sawa na 18.02%, kiyeyusho /j/ kwa kiasi cha 78, sawa na 19.25% na kiyeyusho /w/ kwa kiasi cha 59, sawa na 14.56%. Jedwali lifuatalo linaonesha utamalaki wa athari za kimofofonolojiakutokana na uchopekaji.

**Jedwali Na.4.2: Idadi ya Athari za Kimofofonolojia kutokana na Uchopekaji**

| **Na.** | **Aina za mchakato wa uchopekaji** | **Idadi ya utokeaji** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| | **Jumla** | **405** | **100** |
| 1 | uchopekaji wa /u/ | 94 | 23.21 |
| 2 | Uchopekaji wa /i/ | 101 | 24.94 |
| 3 | Uchopekaji wa /h/ | 73 | 18.02 |
| 4 | uchopekaji wa /j/ | 78 | 19.26 |
| 5 | Uchopekaji wa /w/ | 59 | 14.57 |

Kulingana na kiasi cha athari za kimofofonolojia za Kirundi katika ujifunzaji wa lugha Kiswahili kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi, inadhihirika kuwa uchopekaji wa irabu /u/ na /i/ unajitokeza kwa kiwango kikubwa.

#### 4.3.1.1 Uchopekaji wa Irabu /u/ na /i/

Wanafunzi wa Kiswahili (L2) wazungumzaji wa Kirundi (L1) huchopeka irabu /u/ na /i/ katika maneno ya Kiswahili sanifu yenye muundo wa silabi funge. Kutokana na hali kwamba Kirundi na Kiswahili ni lugha ambishi bainishi, aghalabu lugha hizi ni zenye miundo ya silabi wazi. Hata hivyo lugha ya Kiswahili huwa na silabi funge hususani katika maneno yenye asili ya Kiingereza na Kiarabu. Kwa mfano daktari, mukhtasari, Alhamisi, shtuka, n.k (Iribemwangi, 2010). Aidha kuna baadhi ya maneno ya Kiswahili ambayo muundo wake wa nje ni wa silabi funge. Maneno haya ni kama vile mtu, mzazi, mgeni, mlango, n.k. Hii ina maana kwamba nomino nyingi za ngeli ya kwanza huwa na mofu {mu-} ya kuwakilisha umoja ambayo ina alomofu{m-} na {mw-}. Tunadai kuwa katika muundo nje wa maneno kama haya

irabu /u/ hudondoshwa katika silabi ya kwanza kutegemea mazingira ya kiisimu iliyomo hususani kabla ya konsonanti halisi.

Katika uchambuzi wa data, mtafiti amegundua kwamba athari za uchopekaji wa irabu /u/ zilifanyika kwa kiasi cha 94, sawa na 23.20% , na uchopekaji wa irabu /i/ kwa kiasi cha 101, sawa na 24.93%  ili kuunda muundo wa silabi unaopendelewa.

Jedwali Na.4.3 linaonyesha  mifano ya uchopekaji wa irabu /u/  kutoka kazi za wanafunzi watafitiwa.

**Jedwali Na.4.3: Mifano ya Uchopekaji wa Irabu /u/**

| **Lugha kadirifu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|
| **Mifano** | **Uwakilishi wa kifonetiki** | **Uwakilishi wa kiothografia** | **Uwakilishi wa kifonetiki** |
| m**u**tu | /mutu/ | Mtu | /mtu/ |
| m**u**geni | /mugeni/ | Mgeni | /mgeni/ |
| m**u**lango | /mulango/ | Mlango | /mlango/ |
| m**u**kurugenzi | /mukurugenzi/ | Mkurugenzi | /mkurugenzi/ |
| m**u**koba | /mukoba/ | Mkoba | /mkoba/ |

Katika lugha ya Kirundi, sauti /u/ ya kiambishi haidondoshwi katika ngeli za MU-WA na MU-MI. Kwa mfano *umuuntu*, *umugeni*,*umuryáango* na mengineyo. Kwa hivyo, nomino za ngeli hizo husalia na sauti hiyo. Wanafunzi wazungumzaji wa Kirundi (L1) hufanya makosa ya kuhamisha kiambishi ngeli “MU-” kutoka lugha mama kwenda Kiswahili.Kutokana na uchambuzi wa data, mifano ya uchopekaji wa irabu /i/ imeonyeshwa katika jedwali Na. 4.4 lifuatalo.

**Jedwali Na.4.4: Mifano ya Uchopekaji wa Irabu /i/**

| **Lugha kadirifu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|
| **Mifano** | **Uwakilishi wa kifonetiki** | **Uwakilishi wa kiothografia** | **Uwakilishi wa kifonetiki** |
| Dak**i**tari | /dakitari/ | Daktari | /daktari/ |
| Nilish**i**tuka | /niriʃituka/ | Nilishtuka | /niliʃtuka/ |
| Al**i**hamisi | /alihamisi/ | Alhamisi | /alhamisi/ |
| mak**i**taba | /makitaba/ | Maktaba | /maktaba/ |
| **I**nje | /inɟe/ | Nje | /n:ɲɟɛ/ |

Kama inavyodhihirika katika mifano hapo juu, wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1) wanaojifunza lugha ya Kiswahili (L2) hutamka na kuandika Kiswahili kwa kuchopeka irabu /i/ kwa maneno ya Kiswahili yenye silabi funge, yaani konsonanti mbili zikifuatana katika neno moja. Wanafunzi hufanya makosa ya kutumia muundo wa silabi wa KI ambao ni wa kawaida katika lugha ya Kirundi. Hili ndilo analosisitiza Iribemwangi (2010) akisema kuwa lugha nyingi hupendelea silabi zenye muundo wa KI. Hali hii husababisha wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1) kutamka Kiswahili (L2) kwa kuchopeka /u/ na /i/ katika maneno ya Kiswahili sanifu.

Massamba (2011) anasema kuwa katika lugha kadhaa (zikiwemo lugha za Kibantu) mwambatano wa sauti za aina moja (kama vile konsonanti+konsonanti au irabu+irabu) haupendelewi sana katika utamkaji wa maneno. Kwa hivyo, inadhihirika kuwa kwa maneno ya lugha ya Kiswahili ambayoyanahusisha mfuatano wa sauti konsonanti, wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi wakiyatamka,irabu inachopekwa ili kuzingatia kanuni ya muundo wa silabi wa KI. Pia, sauti inachopekwa kwa ajili ya kuzuia konsonanti kufuatana. Hali hii ndiyo imehamishwa kwenda katika Kiswahili kwa njia inayoleta kasoro.

#### 4.3.1.2 Uchopekaji wa Sauti /h/

Kutokana na uchanganuzi wa data ya kimazungumzo na kimaandishi ya wanafunzi wa Kiswahili wa jamiilugha ya Kirundi kama L1, uchopekaji wa sauti /h/ ulijitokeza kwa kiwango cha kiasi cha 73, sawa na 18.02%. Kutokana na data zilizochanganuliwa , baadhi ya maneno yaliyodhihirisha kasoro hiyo ya uchopekaji wa sauti /h/ yanaoneshwa katika Jedwali Na. 4.5 lifuatalo.

**Jedwali Na. 4.5: Mifano ya Uchopekaji wa Sauti /h/**

| **Lugha kadirifu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|
| **Mifano** | **Uwakilishi wa kifonetiki** | **Uwakilishi wa kiothografia** | **Uwakilishi wa kifonetiki** |
| Hasubui | /hasubui/ | Asubuhi | /asubuhi/ |
| Hofisi | /hofisi/ | Ofisi | /ofisi/ |
| Hasante | /hasante/ | Asante | /asantƐa/ |
| Sina akika | /sina akika/ | Sina hakika | /sina hakika/ |
| Nahuri | /nahuri/ | Nauli | /nauli/ |
| Muzehe | /muzehe/ | Mzee | /mzee/ |
| Saha tatu | /Saha tatu/ | Saa tatu | /saatatu/ |

Kutokana na mifano iliyomo katika jedwali Na. 4.5 ni dhahiri kuwa wanafunzi wa Kiswahili wazungumzaji wa Kirundi huchopeka sauti /h/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu. Kirundi na Kiswahili zina sauti /h/; hivyo si ngeni kwa wanafunzi hawa wanapojifunza Kiswahili. Uchopekaji wa sauti hii katika maneno ya Kiswahili kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi aghalabu hudhihirika kiothografia. Kama inavyodhirika katika mifano, kuna uchopekaji wa /h/ mwanzoni mwa maneno, na katika irabu mbili zinazofuatana katika neno la Kiswahili.

Kasoro ya kuchopeka sauti /h/ mwanzoni mwa maneno ya Kiswahili yanayoanza na irabu hutokana na matamshi ya wazawa wengi wa lugha ya Kirundi. Mara nyingi /h/ huongezwa mwanzoni wakati wa kutamka maneno ya aina hiyo. Kasoro hiyo ndiyo huhamishwa kwenye maandishi kama ilivyotokea katika insha za watafitiwa wazungumzaji wa lugha ya Kirundi.

Kutokana na kasoro ya uchopekaji wa /h/ kati ya irabu mbili, wanafunzi wa Kiswahili wazungumzaji wa Kirundi hujaribu sana kuepuka mfuatano wa sauti irabu katika Kiswahili kama ilivyo katika L1 yao. Kama ilivyoelezwa hapo awali, lugha ya Kirundi inapendelea muundo wazi wa silabi na hakiruhusu mfuatano wa sauti irabu. Wao hufanya hivi kwa kuchopeka sauti /h/ kati ya irabu mbili. Aghalabu uchopekaji huu wa sauti hizo hulenga kuivunja mifuatano ya irabu katika Kiswahili sanifu. Hali hii ni usukukaji wa L1 unaofanyika na wanafunzi hawa ili kuhawilisha muundo wa silabi unaopendelewa na L1 hadi LL.

**4.3.1.3 Uchopekaji wa Viyeyusho /j/ , /w/**

Katika insha za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi watafitiwa wa jamiilugha ya Kirundi, maneno mbalimbali yaliendelezwa vibaya kutokana na uchopekaji wa sauti /j/ na /w/ zisizohitajika katika Kiswahili sanifu.Uchanganuzi wa data ulidhihirisha athari za kuchopeka kiyeyusho /j/ kwa kiwango cha 78, sawa na 19.26%, na za uchopekaji wa kiyeyusho /w/ kwa kiwango cha 59, sawa na 14.56%. Athari za uchopekaji wa viyeyusho zilizojitokeza husababishwa na miundo ya Kirundi. Kirundi hupendelea miundo ya silabi wazi. Sababu huwa ni kuepuka mfuatano wa irabu mbili ili kuunda muundo wa silabi uliopendelewa.

**a) Uchopekaji wa Kiyeyusho /j/ Kiothografia**

Uchopekaji wa sauti /j/ katika maneno ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wazungumzaji wa Kirundi hudhihirika kiothografia. Kihore na wenzake (2008) wanafasili neno othografia kuwa lina asili ya kigiriki na maana yake ni utaratibu wa kutumia alama na michoro ya maandishi kuwakilisha sauti zisikikazo katika lugha. Kila lugha ina mfumo tofauti wa usemaji na hutumia mfumo tofauti wa sauti, na haina budi kubuni mfumo wake wa kuziwakilisha sauti zake katika maandishi. Kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi linganishi tumebaini kuwa wanafunzi wa Kiswahili (L2) wa jamiilugha ya Kirundi (L1) hupendelea uchopekaji wa kiyeyusho /j/. Jedwali Na. 4.6 lifuatalo linaonesha mifano ya sentensi zilizonukuliwa kutoka kazi za wanafunzi kudhihirisha uchopekaji wa kiyeyusho /j/.

**Jedwali Na. 4.6: Mifano ya Uchopekaji wa Kiyeyusho /j/ Kiothografia**

| **Lugha kadirifu** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| **Kiyo** cha bibi harusi kilianguka na kuharibika vibaya. | **Kioo** cha bibi harusi kilianguka na kuharibika vibaya. |
| Nauli ni fedha **inayolipiya** gharama ya safari. | Nauli ni fedha **inayolipia** fedha ya safari. |
| **Chajiyo** ni chakula kinacholiwa **jiyoni**. | Chajio ni chakula kinacholiwa jioni. |
| **Endeleya ninayipenda** hadithi hiyo | **Endelea ninaipenda** hadithi hiyo |
| **Niliyenda** shuleni | N**ilienda** shuleni. |

Jedwali Na. 4.6 linaonesha lugha kadirifu ya mwanafunzi inayodhihirisha baadhi ya maneno yenye uchopekaji wa kiyeyusho /j / wakati mwanafunzi alipokuwa anazungumza au kuandika kiswahili na maneno hayo yanalinganishwa na maneno sahihi katika Kiswahili sanifu.

**b) Uchopekaji wa kiyeyusho /w/ Kiothografia**

Wanafunzi wa Kiswahili (L2) wa jamiilugha ya Kirundi (L1) hukumbwa na uchopekaji wa kiyeyusho /w/ wanapojifunza Kiswahili. Hali hii inasababishwa na miundo ya silabi ya Kirundi. Kirundi hupendelea miundo ya silabi wazi.

Uchanganuzi wa data ulidhirisha kosa la uchopekaji wa kiyeyusho /w/ kimaandishi. Baadhi ya maneno yaliyodhihirisha kasoro hiyo ya uchopekaji wa kiyeyusho /w/ yanaoneshwa katika jedwali Na. 4.7 lifuatalo.

**Jedwali Na. 4.7: Mifano ya Uchopekaji wa Kiyeyusho /w/ Kiothografia**

| **Lugha kadirifu** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| **Funguwa** mlango wa dirisha | **Fungua** mlango wa dirisha |
| Mzee Kasorogani amesema kwamba **atawoga** mwaka **ujawo.** | Mzee Kasorogani amesema kwamba **ataoga** mwaka **ujao.** |
| **Nguwo** za watoto huhifadhiwa | **Nguo** za watoto huhifadhiwa |
| **Mvuwa** im**ebomowa** nyumba nyingi sana. | **Mvua** imebomoa nyumba nyingi sana. |
| Mimi nilizaliwa **mkowani** Gitega. | Mimi nilizaliwa **mkoani** Gitega. |

Jedwali Na. 4.7 linaonesha mifano ya lugha kadirifu ya mwanafunzi yenye baadhi ya maneno yanayodhihirisha uchopekaji wa kiyeyusho/w/ wakatimwanafunzi alipokuwa anazungumza au kuandika Kiswahili (L2). Maneno hayo yanalinganishwa na maneno sahihi katika Kiswahili sanifu.

### 4.3.2 Udondoshaji wa konsanti /h/

Udondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio katika neno kwa njia ambayo inakiuka taratibu za lugha husika. Habwe na Karanja (2007) wanasema kwamba, mfanyiko huu unahusu kuachwa nje kwa sauti fulani ya neno ili kuoanisha matamshi yake. Tofauti katika utaratibu wa mfuatano wa sauti katika uundaji wa maneno kati ya

lugha ya Kirundi (L1) na ile ya Kiswahili (L2) zilisababisha kudondoshwa kwa sauti /h/ kwa njia iliyoleta kasoro katika maneno mbalimbali. Kutokana na data za kimazungumzo na kimaandishi tulizochanganua, baadhi ya wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1) walidondosha sauti /h/ katika kutamka baadhi ya maneno ya Kiswahili (L2) na kisha kupata miundo isiyo sahihi. Kosa la udondoshaji lilidhihirika kwa kiasi cha 102, sawa na 10.01% ya makosa yote yaliyodhihirika katika kazi zilizochambuliwa kama jedwali Na. 4.8 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 4.8: Idadi ya Hali ya Utokeaji wa Udondoshaji wa /h/**

| **aina ya makosa** | **idadi ya makosa** | **asilimia** |
|---|---|---|
| **jumla ya makosa yote** | **1018** | **100** |
| udondoshaji wa /h/ | 102 | 10.019 |

Baadhi ya wanafunzi wakiswahiliwazungumzaji wa Kirundi wanatatizwa na matumizi ya sauti /h/ wanapojifunza Kiswahili. Japo sauti hii inapatikana katika L1 yao, inawatatiza mno katika ujifunzaji wao wa Kiswahili kama L2.

Jedwali Na. 4.9 lifuatalo linaonesha mifano inayodhihilisha kasoro hiyo ya udondoshaji wa sauti /h/ kutokana na data mtafiti alizochanganua.

**Jedwali Na.4.9: Mifano ya Udondoshaji wa /h/**

| **Lugha kadirifu** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| **Mifano** | **Uwakilishi wa kiothografia** |
| Kwa **ivyo** mimi na baba tulienda hospitalini | Kwa **hivyo** mimi na baba tulienda hospitalini. |
| Mbuzi **amsini** walikufa kutokana na mafuriko. | Mbuzi **hamsini** walikufa kutokana na mafuriko.. |
| Mvua iliyonyesha **uyu** mwaka ilikuwa nyingi sana. | Mvua iliyonyesha mwaka **huu** ilikuwa nyingi sana. |
| **Ujambo?** | **Hujambo?** |
| **Ivyo** tulivyosikia | **Hivyo** yulivyosikia |

Jedwali Na. 4.9 linaonesha lugha kadirifu ya mwanafunzi na lugha sahihi.Wanafunzi walidondosha konsonanti /h/ kutoka katika baadhi ya maneno walipokuwa wanazungumza au kuandika Kiswahili.

Udondoshaji wa konsonanti "h" kutoka katika maneno ya Kiswahili inapohusika husababisha wengi kuchanganyikiwa na kukosa kujua waitumie sauti hiyo wapi. Matamshi au maandishi yasipokuwa sahihi kwa neno linalokusudiwa, matokeo wakati mwingine husababisha ujumbe kufika kwa msikilizaji au mpokeaji ukiwa tofauti na kusudi lake na hivyo kusababisha jambo kutotekelezeka kwa usahihi au kutekelezwa tofauti. Mfano kama mtu analenga kusema'Ndugu yako hana watoto' akisema 'Ndugu yako ana watoto'. Udondoshaji huu unaleta utata. Hivyo mawasiliano fanisi yanategemea matamshi na maandishi sahihi ya maneno**.**

### 4.3.3 Matumizi ya Ubadala

Athari za kimofofonolojia zimeibuka katika kazi zote  za watafitiwa mtafiti alizochanganua. Miongoni mwa athari hizi, kuna zile zinazohusu utumiaji wa ubadala usiofaa. Wanafunzi wa Kiswahili (L2)  wazungumzaji wa Kirundi (L1)

hutatizwa na utamkaji au uandikaji wa Kiswahili kutegemea muundo wa kiisimu wa L1 yao. Uchambuzi wa data za watafiwa wanafunzi umedhihirisha athari za kimofofonolojia kwa kutumia ubadala kwa kiasi cha 511, sawa na 50.19% ya athari zote za kimofofonolojia zilizoonekana katika kazi za Kiswahili za wanafunzi watafiwa zilizochanganuliwa na mtafiti. Miongoni mwa aina hii ya matumizi ya ubadala, kuna aina mbalimbali za matumizi ya konsonanti mbadala kama jedwali Na. 4.10 lifuatalo linavyodhihirisha.

**Jedwali Na. 4.10 : Aina na Idadi ya Athari za Matumizi ya Konsonanti Mbadala**

| **Na** | **Aina za makosa ya matumizi ya fonimu mbadala** | **Idadi ya utokeaji** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| | **Jumla** | **511** | **100** |
| 1 | konsonanti /β/ badala ya /b/ | 39 | 7.63 |
| 2 | konsonanti /c/ badala ya /ch/ | 32 | 6.26 |
| 3 | konsonanti /g/ badala ya /ɤ/ | 141 | 27.59 |
| 4 | konsonanti /r/ badala ya /l/ | 57 | 11.15 |
| 5 | konsonanti /z/ badala ya /ð/ | 117 | 22.90 |
| 6 | konsonanti /f/ badala ya /ɵ/ | 26 | 5.09 |
| 7 | konsonanti /s/ badala ya /ɵ/ | 99 | 19.37 |

Katika Jedwali Na. 4.10 hapo juu inaonekana kuwa kuna athari katika matumizi ya konsonati mbadala. Miongoni mwa athari hizo kuna matumizi ya konsonanti/β/ badala ya /b/ kwa kiasi cha makosa 39, sawa na 7.63%, /c/ badala ya /ch/ kwa kiasi cha 32, sawa na 6.26%, /g/ badala ya /ɤ/kwa kiasi cha 141, sawa na 27.59%, /r/ badala ya /l/ kwa kiasi cha 57, sawa na 11.15%, konsonanti /z/ badala ya /ð/ kwa kiasi cha 117, sawa na 22.90%, konsonanti /f/ badala ya /ɵ/ kwa kiasi cha 26, sawa na 5.09% , na matumizi ya konsonanti /s/ badala ya /ɵ/ kwa kiasi cha 99, sawa na 19.37%.

Tatizo hili ni sugu miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa jamiilugha ya Kirundi (L1), wanatatizwa na utamkaji au uandishi wa LL kutegemea muundo wa kiisimu wa L1 yao. Konsonanti za Kirundi (L1) zinafanana sana na zile za Kiswahili (L2) kwa kiasi kikubwa. Kirundi (L1) na Kiswahili (L2) ni lugha za nasaba moja lakini mifumo ya konsonanti inafanana kwa asilimia sabini na sita (76%). Tunaweza kusema kwamba hali hii imesababishwa na ukopaji mpana wa msamiati unaokumba kiswahili sanifu.

#### 4.3.3.1 Matumizi ya /β/ badala ya /b/

Uchambuzi wa data za kimazungumzo ulionesha kuwa wanafunzi wengi wametumia konsonanti /β/ mahala pa konsonanti /b/ kimatamshi. Wanafunzi hutamka konsonanti /β/ ambayo ni kikwamizwa ghuna cha midomo cha Kirundi (L1) mahala pa konsonanti /b/ katika Kiswahili (L2). Wanafunzi wa Kiswahili (L2) wazungumzaji wa Kirundi (L1) hukanganywa sana na utamkaji wa konsonanti /β/ na /b/.

Utafiti huu ulidhihirisha makosa 39, sawa na 7.63% ya matumizi ya konsonanti /β/ badala ya /b/ kwa jumla ya makosa 511 ya matumizi ya konsonanti mbadala. Mifano ya maneno yanayodhihirisha kasoro hiyo ni katika jedwali Na. 4.12.

**Jedwali Na. 4.12: Mifano ya Matumizi ya /β/ badala ya /b/**

| **Lugha kadirifu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|
| Mifano | Uwakilishi wa kifonetiki | Uwakilishi wa kiothografia | Uwakilishi wa kifonetiki |
| Karibu | /kari**βu/** | Karibu | /karibu/ |
| Bahati nzuri | **/βahati/** | Bahati | /bahati/ |
| Hodi Babu | **/ hodi βaβu/** | Hodi Babu | / hodi babu/ |

#### 4.3.3.2 Matumizi ya ‘c’ badala ya ‘ch’

Matumizi ya sauti /ʧ/ ambayo hunukuliwa kiothografia kama ‘c’ katika Kirundi na ‘ch’ katika Kiswahili huwatatiza wanafunzi wazungumzaji wa Kirundi (L1) wanapojifunza Kiswahili (L2). Kosa la utumiaji wa herufi ‘c’ badala ya ‘ch’ lilijitokeza mara 32, sawa na 6.26% ya jumla ya makosa ya matumizi ya konsonanti mbadala. Ukosekanaji wa ‘ch’ katika lugha ya Kirundi (L1) umedhihirika katika kazi andishi za wanafunzi watafitiwa. Wanafunzi wa Kiswahili (L2) wa jamiilugha ya Kirundi (L1) wanashindwa kutumia herufi ‘ch’ ambayo ni ngeni kwao na badala yake huandika ‘c’. Jedwali Na. 4.12 lifuatalo linadhihirisha baadhi ya mifano ya matumizi ya ‘c’ badala ya ‘ch’.

**Jedwali Na. 4.12: Mifano ya Matumizi ya ‘c’ badala ya ‘ch’ Kiothografia**

| **Lugha kadirifu** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| **Cajio** ni **cakula kinacoliwa** jioni | **Chajio** ni **chakula kinacholiwa** jioni |
| **Ca** mlevi huliwa na mgema | **Cha** mlevi huliwa na mgema |
| **Cayi** ya dakitari imemwangika | **Chai** ya daktari imemwangika |
| **Cakula** kimeyiva | **Chakula** kimeiva |
| Leta cumvi. | Leta **chumvi** |

Herufi ‘ch’ haipatikani katika Kirundi na badala yake ‘c’ iliyo ghuna na inayotamkiwa kwenye kaakaa gumu kama ilivyo ‘ch’ ndiyo hutumika sana miongoni mwa wazungumzaji wa Kirundi (L1) wanapojifunza Kiswahili (L2).

#### 4.3.3.3 Matumizi ya Konsonanti /g/ badala ya /ɣ/

Uchambuzi wa data za kimatamshi na kimaandishi unaonesha kuwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi wanapendelea sana kutamka sauti /g/ inayopatikana katika L1 yao mahala pa /ɣ/ kwa kiasi cha 141, sawa na 27,59% katika jumla ya athari zote za

matumizi ya konsonanti mbadala**.** Sauti /ɤ/ haimo kwenye mfumo wa sauti za Kirundi. Kwa hivyo, sauti /g/ ambayo pia hutamkwa kwenye kaakaa laini huchukua nafasi ya /ɤ/ wanapotumia Kiswahili. Sauti hizo mbili hutamkiwa kwenye sehemu sawa ya kinywa ingawa moja ni ya Kipasuo ilhali nyingine ni kikwamizwa. Maana hupotea katika hali hii. Hata hivyo, maana wakati mwingine haipotei hasa anayezungumziwa akielewa jinsi mtumizi huyu wa Kiswahili anavyohamisha mfumo wa sauti za L1 yake. Baadhi ya wanafunzi wa Kirundi walishindwa kuendeleza ifaavyo maneno yenye sauti /ɤ/ kutokana na uhawilishaji kama jedwali Na. 4.13 lianaonesha mifano ya kosa la matumizi ya konsonanti/g/ badala ya / ɤ /.

**Jedwali Na. 4.13: Mifano ya Kiothografia ya Matumizi yaKonsonanti /g/ Badala ya /ɤ/**

| **Lugha kadirifu** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| Wakati wa masika, mvua ilikuwa nyingi mno hadi **magorofa** kando ya ziwa Tanganyika yakafurikwa. | Wakati wa masika, mvua ilikuwa nyingi mno hadi **maghorofa** kando ya ziwa Tanganyika yakafurikwa. |
| Nauli ni feza unayolipia **garama** ya safari | Nauli ni feza unaolipia **gharama** ya safari |
| Mimi ninazungumza **luga** ya Kirundi | Mimi ninazungumza **lugha** ya Kirundi |

Mifano hapo awali inaonesha lugha kadirifu ya mwanafunzi na lugha sanifu. Wanafunzi wa Kiswahili (L2) wanafanya makosa hayo kwa sababu lugha ya Kirundi (L1) ina konsonanti /g/ tu ilhali Kiswahili kina konsonanti zote /g/ na / ɤ /. Ukosefu wa konsonanti /ɤ/ katika L1 ya wanafunzi husababisha hawa wapate ugumu kutamka au kuandika konsonanti hiyo katika L2. Wanafunzi hawa huhawilisha lugha pale ambapo kuna konsonanti ngeni kwao /ɤ/ na badala yake kuandika konsonanti /g/ jirani kiisimu kutoka L1 yao.

#### 4.3.3.4 Matumizi ya Konsonanti /r/ badala ya /l/

Katika kazi zilizochanganuliwa na mtafiti miongoni mwa konsonanti zilizobadilishana nafasi, kuna konsonanti /r/ na /l/ kwa kiasi cha 57, sawa na 11.15% kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

Matumizi ya /r/ badala ya /l/ katika mifano hiyo hapo juu, yalitokana na ukweli kwamba katika lugha ya Kirundi hakuna sauti /l/. Wanafunzi husika walitumia sauti wanayoifahamu /r/; na hivyo kuleta kasoro katika maneno ya Kiswahili yahusishayo konsonanti /l/. Hali iliyo kinyume na hiyo ilijitokeza katika mifano mitatu ya mwisho ambapo watafitiwa walitumia /l/ mahali ambapo walistahili kutumia /r/. Kasoro hii ilisababishwa na Kuimarika kwa konsonanti. Mfanyiko huu huhusu likwidi /l/ na /r/. Dhana ya kuimarika inarejelea hali ya sauti ambayo kwa kawaida hutamkwa kwa nguvu kidogo kubadilika na kuwa ya kutamkwa kwa nguvu nyingi.

Insha zilizoandikwa na watafitiwa wazungumzaji wa Kirundi (L1) zilidhihirisha athari ya lugha hiyo kupitia ubadilishaji wa konsonanti /r/ na /l/ katika maneno anuwai. Mifano ya maneno yanayodhihirisha kasoro hiyo inaonekana katika jedwali Na. 4.14

**Jedwali Na.4.14: Mifano ya matumizi ya Konsonanti/r/ badala ya /l/**

| **Lugha kadirifu** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| **Mifano** | **Uwakilishi wa kiothografia** |
| Fungua **murango** wa dirisha | Fungua **mlango** wa dirisha |
| **Nauri** ni feza **unayoripiya** gharama ya safari | **Nauli** ni feza **unaolipia** gharama ya safari |
| Maktaba ni **mahari** ambapo vitabu na vifaa vinavyohusika na **erimu** vinahifadhiwa ili wasomji wavitumie . | Maktaba ni **mahali** ambapo vitabu na vifaa vinavyohusika na **elimu** vinahifadhiwa ili wasomji wavitumie. |

Wanafunzi wa kiswahili wazungumzaji wa Kirundi hutatizwa mno na matumizi ya konsonanti /r/ na /l/. Hali hii husababishwa na ukosefu wa konsonanti /l/ katika L1 yao, Kirundi kina kimandende /r/. Kwa sababu hii wanafunzi wengi hukanganyika wasijue jinsi ya kutumia fonimu hizi mbili ipasavyo. Matatizo hutokea pale sauti inayotumiwa katika Kiswahili ni /l/. Hivyo mwanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1) hutumia konsonanti /r/ badala ya /l/ azungumzapo Kiswahili (L2).

#### 4.3.3.5 Matumizi ya Konsonanti/z/ badala ya /ð/

Uchanganuzi wa data ulionesha kwamba aina ya kosa la kutumia konsonanti /z/ badala ya /ð/ lilijitokeza kwa kiasi cha 117, sawa na 22.90% miongoni mwa jumla ya athari za kimofofonolojia katika matumizi ya sauti mbadala. Mifano inayodhihirisha kasoro hiyo ni hii katika jedwali Na.4.15.

**Jedwali Na. 4.15: Mifano ya Kiothografia ya Matumizi ya /z/ badala ya /ð/**

| **Lugha kadirifu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|
| **Mifano** | **Uwakilishi wa kifonetiki** | **Uwakilishiwa kiothografia** | **Uwakilishi wa kifonetiki** |
| Afazari | /afazari/ | Afadhali | /afaðali/ |
| Feza | /feza/ | Fedha | /feða/ |
| Bizaa | /biza:/ | Bidhaa | /biða:/ |
| kuhifaziwa | /Kuhifaziwa/ | Kuhifadhiwa | /kuhifaðiwa/ |
| zambi | /zambi/ | Dhambi | /ðambi/ |

Wanafunzi wa Kiswahili (L2) wazungumzaji wa Kirundi (L1) hutatizwa mno kimatamshi na matumizi ya konsonanti /z/ mahala pa konsonanti /ð/. Ijulikane kwamba lugha ya Kirundi haina sauti /ð/. Hivyo basi, ukosefu wa konsonanti hii katika L1 ya wanafunzi hawa ni kizuizi hasa cha utamkaji na uandikaji faafu katika

Kiswahili (L2). Badala ya konsonanti hiyo wanafunzi huishia kutumia konsonanti ambayo inapatikana katika L1 yao mahala pa konsonanti /ð/ ya L2. Kukanganywa huku kunaletwa na mchakato wa uhawilishaji lugha. Tatizo la kuhaulisha mfumo wa L1 ya mwanafunzi hadi L2 ni sugu mno miongoni mwa wanafunzi wengi. Tunaweza kusema kwamba wengi wa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1) hushindwa kabisa kumudu matamshi ya Kiswahili (L2). Hata hivyo, kuna baadhi ya wanafunzi ambao hupendelea kutumia konsonanti /ð/ ambayo ni ngeni kwao badala ya /z/ ambayo ni asili katika Kirundi. Wanafunzi hawa hufanya hivyo kama mkakati wao wa kufanikisha mawasiliano kupitia Kiswahili ambacho ni L2 yao.

#### 4.3.3.6 Matumizi ya /s/ badala ya /ɵ/

Uchambuzi wa data unadhihirisha athari ya lugha ya Kirundi (L1) kupitia ubadilishaji wa konsonanti /ɵ/ katika maneno anuwai na kutumia konsonanti /s/ badala yake.Kosa hili lilitokea kwa kiasi cha 99 sawa na 19.37% ya jumla ya athari za kimofofonolojia katika matumizi ya konsonanti mbadala.Mifano ya baadhi ya maneno yenye kasoro hii yameoneshwa katika jedwali Na. 4.16.

**Jedwali Na. 4.16: Mifano ya Matumizi ya Konsonanti/s/ badala ya /ɵ/**

| **Lugha kadirifu** | | **Kiswahili sanifu** | |
|---|---|---|---|
| **Mifano** | **Uwakilishi wa kifonetiki** | **Uwakilishi wa kiothografia** | **Uwakilishi wa kifonetiki** |
| Serasini | /serasini/ | Thelathini | / ɵɛlaɵini / |
| Samani | /samani/ | Thamani | / ɵamani / |
| Semanini | /semanini/ | Themanini | /ɵɛmanini/ |

Mfumo wa konsonanti za Kirundi hauna sauti /ɵ/. Kwa hiyo mzungumzaji ambaye anazungumza Kirundi (L1), anapotumia Kiswahili (L2) anadhihirisha athari za sauti

nyingine katika kuitamka sauti hii. Sauti /ɵ/ ni ya ulimi na meno na sighuna. Kwa hivyo sauti ya Kirundi ambayo sighuna ni /s/ inayotamkwa wakati ncha ya ulimi na ufizi hukaribiana. Kisha kuruhusu hewa kupita kwa kukwamizwa.

#### 4.3.3.7 Matumizi ya Konsonanti /f/ badala ya /ɵ/

Uchanganuzi wa kazi za watafitiwa wanafunzi ulidhihirisha athari ya matumizi ya konsonanti /f/ badala ya konsonanti /ɵ/. Kosa hili limetokea kwa kiasi cha 26, sawa na 5.09% ya jumla athari zote za kimofofolojia katika mchakato matumizi ya konsonati mbadala. Mifano ya baadhi ya maneno yenye upungufu huu yalioneshwa katika jedwali Na. 4.17%.

**Jedwali Na.4.17: Mifano ya Matumizi ya Konsonanti/f/ badala ya /ɵ/**

| **Lugha kadirifu** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| **Mifano** | **Uwakilishi wa kiothografia** |
| Endelea ninaipenda **hadifi** hiyo | Endelea ninaipenda **hadithi** hiyo |
| Nyumba **felafini** na tano zilibomoka wakati wa mafuriko | Nyumba **thelathini** na tano zilibomoka wakati wa mafuriko |

Jedwali Na. 4.17 la hapo juu linaonyesha kwamba wanafunzi wa Kiswahili (L2) wazungumzaji wa Kirundi (L1) wanatatizwa mno na matumizi ya konsonanti /ɵ/ katika uamiliaji wa Kiswahili (L2). Kwa hivyo, wanatumia konsonanti /f/ badala ya konsonanti **/ɵ/.** Tukumbuke kwamba Kirundi hakina konsonanti **/ɵ/**. Ukosefu huu katika Kirundi (L1), husababisha maandishi yasiyofaa ya maneno ya Kiswahili, yenye konsonanti **/ɵ/** katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2). Wanafunzi hupendelea kutumia konsonanti /f/ ambayo inapatikana katika L1 yao badala ya /ɵ/ kimaandishi au kimatamshi. Kukanganywa huku kunasababisha wanafunzi hawa kuhawilisha sauti kutoka L1 yao hadi Kiswahili (L2).

Katika sehemu hii, mtafiti alishughulikia malengo ya kwanza na pili ya utafiti huu. Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1), na lengo la pili ni kutathmini viwango vya utamalaki wa aina mbalimbali za athari za kimofofonolojia ya Kirundikatika ujifunzaji wa Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1). Baada ya uchanganuzi wa data, mtafiti aligundua kuwa kuna aina kuu tatu michakato ya athari za Kimofofonolojia yaliyojitokeza katika matumizi ya maneno mbalimbali katika matamshi na uandishi insha. Michakato iliyoshughulikiwa ni udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa sauti. Hii ni hali ambayo hujitokeza kutokana na haja ya watafitiwa husika kutaka kurahisisha ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili (L2) kwa kutumia misingi ya Kirundi kama L1 yao.

Kulingana na kazi tangulizi zilizoshughulikia athari za L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2, ni dhahiri kuwa utafiti huu unashabihiana na baadhi ya kazi hizo. Kwa mfano, Massamba (1986), katika kuchunguza athari za lugha mama katika Kiswahili Mkoani Mara nchini Tanzania. Aligundua kuwa lugha za kienyeji na lugha ya Kiswahili ziliathiriana. Katika fonolojia, Massamba alionesha jinsi sauti zilivyoongezwa au kudondoshwa katika maneno ya Kiswahili kutokana na athari ya L1, hali iliyosababisha makosa ya utamkaji.

Otiende (2013) naye, akiangazia athari zinazodhihirika kimatamshi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba wanapotumia Kiswahili, aligundua kuwa athari za mofofonolojia ya Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili husababishwa na sauti za Kiswahili zisizopatikana katika Kiolusuba na miundo tofauti ya baadhi ya maneno.

Pia, katika utafiti wake, Nyanda (2015) alichunguza athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza Kiswahili, utafiti wake umedhihirisha athari hizo katika nyanja za isimu, za msamiati, matamshi na maana. Kwa upande wa matamshi, alibaini ya kwamba baadhi ya wanzungumzaji wa Kinyamwezi wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya kubadili matamshi sahihi ya sauti wakati wanapotamka neno na badala yake kutumia matamshi yasiyo sahihi. Baadhi ya wazungumzaji wa Kinyamwezi huchopeka silabi mojawapona pia hudondosha baadhi ya sauti wakati wa ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili watoapo sentensi za Kiswahili.

Naye Mashaka (2015) akichunguza Athari za lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi, aligundua kuwa athari za matamshi zinazojitokeza kwa wanafunzi wanapojifunza lugha ya Kiswahili ni pamoja na udondoshaji wa sauti, kutumia sauti zinazokaribiana na kuongeza viambishi visivyohitajika.

Kazi tangulizi zilizoshughulikia athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa kiswahili kama L2 zinafanana sana na kazi hii. Tafiti za awali zinahakikisha kuwa athari za L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 zinasababisha makosa ya kimofofonolojia

Kwa ujumla, ufanano uliopo baina ya tafiti tangulizi na utafiti huu ni kuelewa athari na aina za kimofofonolojia ya L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2. Imedhihirika kwamba wazawa wa lugha anuwai za Kibantu huendeleza maneno ya Kiswahili kwa njia isiyo sahihi kutokana na uhamishaji wa mifumo ya kifonolojia kutoka L1 zao. Tofauti iliyopo ni kuwa tafiti hizo tangulizi hazikushughulikia pamoja data za kimatamshi na za kimaandishi kama utafiti huu ulivyofanya.

## 4.4 Juhudi za Walimu Kubaini na Kukabiliana na Athari kimofofonolojia za Kirundi katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama L2.

Katika sehemu hii mtafiti alikusudia kuwasilisha data za lengo mahususi la tatu la utafiti huu ambalo lililenga kubainisha juhudi mbalimbali za walimu kubaini na kukabiliana na aina za athari za kimofofonolojia za Kirundi (L1) katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2). Lengo hili la tatu lilishughulikiwa kwa njia ya kuchanganua majibu yaliyotolewa na watafitiwa walimu wa Kiswahili. Watafitifitiwa hawa walikuwa wanane na kila mmoja alipatiwa nakala ya hojaji kwa walimu. Baada ya kukusanya na kuchanganua data zilizotokana na hojaji hiyo, ilionekana kwamba mbinu zilizotolewa na walimu watafitiwa ni kama mwongozo wa kufundishia na kuwasaidia wanafunzi ili wazoee kuongea na kuandika Kiswahili. Mwongozo huu unategemea stadi nne za ujifunzaji yaani: usikivu, usomaji, uandishi na usemaji. Kila stadi ya ujifunzaji ina mbinu zake kama watafitiwa walimu walivyoeleza.

Kwa ujumla, mbinu zilizotolewa na walimu watafitiwa ili kukabilana na athari za mofofonolojia pamoja na kuwasaidia wale ambao tayari waliathirika na lugha mama ya Kirundi katika kujifunza lugha ya Kiswahili zimeoneshwa katika jedwali Na. 4.18.

**Jedwali Na. 4.18: Mbinu za walimu kubaini na kukabiliana na athari za mofofolojia**

| Na. | Stadi za ujifunzaji | Mbinu za walimu kubaini na kukabiliana na athari za mofofonolojia | Idadi ya watafiwa waliopendekeza | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Usikilizaji | Mwalimu anasoma aya fupifupi na kuuliza wanafunzi maswali ya ufahamu. | 5 | 62.5 |
| | | Mwalimu anasoma aya nzima na kuuliza wanafunzi maswali ya ufahamu. | 5 | 62.5 |
| | | Mwalimu anawasomea wanafunzi matini polepole (imla) na wao wakaandika. | 6 | 75 |
| 2 | Uzungumzaji | Mwalimu anawaambia wanafunzi kusimulia habari na kisha anaandika makosa ubaoni. | 7 | 87.5 |
| | | Mwalimu anaanza kupitia kosa baada ya jingine kwa kuuliza wanafunzi usahihi wa kila neno. | 5 | 62.5 |
| | | Mwalimu anafuta kosa na anaandika usahihi wa neno ubaoni. | 3 | 37.5 |
| 3 | Usomaji | Mwalimu anawapa wanafunzi kazi ya usomaji na kujaribu kuelewa habari. | 6 | 75 |
| 4 | Uandishi | Mwalimu anawambia wanafunzi kuandika habari yoyote kuhusu mada fulani. | 6 | 75 |
| | | Mwalimu anaambia kila mwanafunzi kusoma alichoandika. | 6 | 75 |
| | | Mwalimu anaandika ubaoni makosa yanayojitokeza. | 6 | 75 |
| | | Mwalimu anawambia wanafunzi kuutafuta usahihi wa makosa yaliyojitokeza. | 6 | 75 |
| | | Baada ya hapo, mwalimu anawaambia wanafunzi kurekebisha makosa na kuandika tena habari hiyo. | 5 | 62.5 |

Watafitiwa walimu walibainisha mbinu mbalimbali wanazotumia kukabiliana na athari za kimofofonolojia na kusaidia wanafunzi walioathirika ili watumie Kiswahili. Kwa upana mbinu hizo zinaelezwa kama ifuatavyo.

### 4.4.1 Usikilizaji

Kutokana na uchambuzi wa data, watafitiwa walimu wa Kiswahili walieleza mbinu wanazotumia ili wakabiliane na athari za kimofofolojia za lugha ya Kirundi (L1) katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2) katika stadi ya usikilizaji.katika stadi hii ya kutumia mbinu ya usikilizaji, matokeo ya data za hojaji yalionesha kwamba watafitiwa walimu 5, sawa na 62.5% wanatumia mbinu ya kusoma aya fupifupi na kisha kuuliza swali la ufahamu. Mwalimu anawaambia wamsikilize, kisha anasoma aya fupifupi na kisha anawauliza swali la kujua wamesikia kitu gani. Hapo mwalimu anawaambia waandike katika madaftari yao kile walichosikia. Na baadaye mwalimu anaambia kila mwanafunzi asome alichoandika. Mwalimu anaandika ubaoni makosa yaliyojitokeza kutokana na miundo ya maneno na sauti zinazowatatiza, na kuyarekebisha. Kisha mmoja mmoja, wanafunzi wanasoma kwa usahihi maneno mwalimu aliyoandika ubaoni. Hapa mwalimu anahakikisha matamshi ya maneno na kurekebisha panapohitajika.

Kutokana na matokeo ya data, walimu 5, sawa na 62.5% walieleza mbinu ya pili wanayotumia katika stadi ya usikilizaji kuwa mwalimu anawasomea wanafunzi aya nzima na baadaye anawauliza maswali yanayotokana na aya aliyowasomea. Wanafunzi wajibu maswali na mwalimu anarekebisha penye makosa.

Pia, uchanganuzi wa data unaonesha kwamba walimu 6, sawa na 75% walieleza mbinu ya tatu inayotumiwa na walimu katika stadi ya usikilizaji, ni kuwa mwalimu

anawasomea matini polepole kama imla na kisha anawaambia wanafunzi waandike. Wakimaliza wanasoma kwa sauti na mwalimu anaandika ubaoni pamoja makosa yanayojitokeza. Wanafunzi wanasoma sentensi zilizoandikwa ubaoni, mwalimu anawaambia wanafunzi warekebishe makosa ubaoni. Kama wameshindwa mwalimu anarekebisha kosa. Mwisho mwalimu anawaambia wazisome sentensi hizo kwa sauti ili aelewe kuwa matamshi yao yamekaa sawasawa .

### 4.4.2 Stadi ya Uzungumzaji au Maongezi

Katika kipindi hiki cha stadi ya uzungumzaji uchambuzi wa data umeonesha kuwa watafitiwa walimu wametofautisha mbinu tatu. Mbinu ya kwanza iliyoelezwa na walimu 7, sawa na 87.5%, ni kuwa mwalimu anawaambia wanafunzi kusimulia habari na kisha anaandika ubaoni makosa ya mofofonolojia ya matamshi wanayofanya. Wakati mwanafunzi anaposimulia, mwalimu anamsikiliza na kuandika makosa yote ubaoni. Mbinu ya pili inayotumiwa na mwalimu ilielezwa na walimu 5, sawa na 62.5%. Mbinu hiyo ni kuwa wanafunzi wakimaliza kusimulia, mwalimu anaanza kupitia kosa moja baada ya jingine kwa kuwaomba wanafunzi kutoa usahihi. Uchanganuzi wa data ulionesha kuwa watafitiwa 3, sawa na 37.5%, walieleza mbinu ya tatu inayotumiwa katika stadi ya uzungumzaji. Katika mbinu hii, mwalimu anafuta kosa na kuandika kilicho sahihi na kuwaomba wasome tena.

Ili kupunguza athari za lugha ya Kirundi (L1), watafitiwa walimu walieleza kuwa wanahimiza wanafunzi kujizoeza kuzungumza na kuandika lugha ya Kiswahili (L2) katika mazingira ya shuleni na nyumbani ili kupata uwezo wa kuongea na kuandika lugha hiyo bila usumbufu wowote. Kwa upande wa watafitiwa,walimu walieleza kwamba wakati wa kufundisha somo la Kiswahili, walimu hawatumii lugha nyingine

ila tu lugha ya Kiswahili (L2) na kukataza wanafunzi kuongea Kirundi (L1) wawapo shuleni. Vilevile kuhimiza matumizi ya Kiswahili wawapo nje ya shule (nyumbani). Watafitiwa walimu walieleza kuwa wanaweka mkazo katika ufundishaji wa somo hili la Kiswahili ili wanafunzi wasiwe na mazoea ya kuongea lugha ya Kirundi wakati wa ufundishaji.

### 4.4.3 Stadi ya Usomaji

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa watafitiwa walimu 6, sawa na 75%, walieleza mbinu ya kuwapa wanafunzi kazi ya usomaji na kujaribu kuelewa habari. Kama walivyoeleza juu ya mbinu wanayotumia katika ustadi huu wa usomaji ili kubaini na kukabiliana na athari za kimofofolojia, mwalimu anawapa wanafunzi kazi ya usomaji na kujaribu kuelewa habari. Baada ya wanafunzi kusoma habari hiyo, mwalimu anatoa mawazo muhimu ya habari hiyo. Kisha anawauliza kama wamekutana na maneno magumu. Wakiwa wanayataja mwalimu anayaandika ubaoni na kuwauliza maana zake. Mwisho, mwalimu anawauliza maswali ya ufahamu ili kupima kama wameelewa walichokisoma au la. Baada ya kazi hii, mwalimu anawaambia wanafunzi wasome tena kwa sauti ili kuhakikisha mikazo, kiimbo na matamshi kama iko mahali sahihi na wanatamka kwa usahihi. Pamoja na hayo, watafitiwa walibaini pia mbinu ya kuwapa wanafunzi mazoezi mengi ya kusoma na kusimulia hadithi za Kiswahili. Katika mbinu hii, walimu watafitiwa walieleza kuwa mazoezi ya usomaji wa vitabu na magazeti, michezo na mijadara yalisaidia kuendeleza mawasiliano na kukuza lugha kwa wanafunzi. Walipendekeza kuwa mbinu hii ikiendelezwa na walimu wengine wa lugha, wanafunzi wataweza kuepukana na athari za lugha ya Kirundi (L1) na kuwa watumiajii wazuri wa lugha ya Kiswahili (L2).

#### 4.4.4 Stadi ya Uandishi

Matokeo za uchambuzi wa data yalionesha kuwa kuna mbinu tano zinazotumiwa katika stadi ya uandishi ili kupunguza athari za lugha ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili. Mbinu ya kwanza iliyoelezwa na watafitiwa 6, sawa na 75%, ni kuwa mwalimu anawambia wanafunzi kuandika habari yoyote kuhusu mada fulani. Wakimaliza, kila mwanafunzi anasoma alichoandika, pamoja na kazi hii, mwalimu anaandika ubaoni makosa yanayojitokeza. Hapa mwalimu anaorodhesha maneno mbalimbali ya Kiswahili yenye sauti zinazowatatiza kimatamshi au kimaandishi. Kisha mwalimu anawaambia wanafunzi kutafuta usahihi wa makosa yaliyojitokeza na kuyarekebisha. Baada ya hapo, mwalimu anawaomba wanafunzi kuandika tena habari nzima hiyo. Mbinu hii inatumiwa kusaidia wanafunzi walioathirika na lugha mama wakati wa ufundishaji. Lengo la kuwapa wanafunzi zoezi hili ni kuwazoeza uandishi katika Kiswahili. Watafitiwa walimu walieleza pia, kuwa wanawapatia wanafunzi kazi nyingi za usomaji wa vitabu na magazeti, michezo na mijadara ili kuendeleza mawasiliano na kukuza lugha kwa wanafunzi. Mbinu hii iliendelezwa ili wanafunzi waweze kuepuka athari za lugha ya Kirundi (L1) na kuwa watumiajii wazuri wa lugha ya Kiswahili (L2).

Kulingana na kazi tangulizi zilizoshughulikia mbinu za ufundishaji wa L2, ni dhahiri kuwa utafiti huu unafanana kwa kiasi kikubwa na kazi hizo tangulizi. Kwa mfano, Richards na Rodgers (1986) wanasema kuwa msingi wa luhga yoyote ile uko katika mazungumzo, kwani mazungumzo ndicho kipengele cha lugha ambacho tunajifunza kabla ya kuweza kusoma na kuandika.

Bruke na Steffen (1994) wanakubaliana na madai haya wakisema kuwa, msingi wa lugha ni kile kinachozungumzwa kisha kuandikwa. Mazungumzo kwanza kabla stadi zinginezo, umilisi wa stadi hizi utategemea mwelekeo mahususi mwalimu atakaoamua kushirikisha wanafunzi wake katika hali mbalimbali za mazungumzo mfano mijadala, mahojiano, hotuba, uigizaji, n.k. Mazungumzo bora huwepo iwapo wanafunzi watatamka sauti ipasavyo.

Gathindi na Matembe (2005) wanasema kuwa ni jukumu la mwalimu wa lugha kuwapa wanafunzi nafasi za kutumia lugha wao wenyewe. Ubora wa usikilizaji utegemea kinachowasilishwa na kinavyowasilishwa. Hivyo basi mwalimu awe daima wa kuigwa daima atoe maagizo mahususi anavyotarajia wanafunzi wafanye baada ya kusikiliza.

Kulingana na Elaessen (1994), akieleza jinsi ya kufunza lugha, anasema kuwa ili mwanafunzi aweze kujifunza kuzungumza, kuandika na kusoma lazima hutumia lugha husika mara kwa mara. Anapendekeza mwanafunzi apewe nafasi ya kufanya marudio na mazoezi mengi. Hili lifanyike katika muktadha wa kifungu au kitabu na siyo kukariri maneno. Vifungu vya aya ndio njia ya pekee ya mwanafunzi kujifunza baadhi ya vipengele vya lugha.

Kutokana na maelezo ya awali, ni dhahiri kuwa mbinu za ufundishaji wa L2 zifuate mkondo wa stadi kuu za lugha yaani usikilizaji, uzungumzaji, usomaji na uandishi.

## 4.5 Hitimisho la Sura ya Nne

Katika sura hii ya nne, mtafiti amejishughulisha na uwasillishaji na uchanganuzi wa data zilizokusanywa uwandani kuhusu athari za kimofofonolojia ya Kirundi (L1)

katika ujinzaji wa Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi. Data hizi zilipatikana kwa kutumia mbinu za hojaji, ushuhudiaji na jaribio la umilisi. Malengo ya utafiti huu yamezingatiwa katika uwasilishaji na uchambuzi wa data. Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi iliongoza utafiti huu. Mikabala ya kitakwimu na kimaelezo ilitumika pamoja. Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ilisaidia katika kuchanganua data na kutoa majibu ya maswali ya utafiti huu. Sura inayofuata ilijikita katika muhtasari, hitimisho namapendekezo.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ilifanya muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti mzima. Utafiti huu ulilenga kuchunguza athari za kimofofonolojia ya Kirundi (L1) katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi.

## 5.2 Muhtasari

Muhtsari umegawanyika katika sehemu mbili tofauti. Muhtasari wa jumla na ule wa matokeo ya utafiti kama ilivyoelezwa hapo chini.

### 5.2.1 Muhtasari kwa Ujumla

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza athari za mofofonolojia ya lugha ya Kirundi (L1) katika uamiliaji wa Kiswahili (L2). Utafiti ulifanyika kwenye vyuo vikuu vitatu vinavyofundisha Kiswahili kama kozi muhimu ya lazima katika mwaka wa kwanza wa shahada ya kwanza: Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu (Université des gands Lacs, UGL), Chuo Kikuu cha Busara ya Afrika (Université Sagesse d’Afrique, USA) na Chuo Kikuu cha Mwaro (Université de Mwaro, UM). Watafitiwa waliohusishwa ni wanafunzi 100 na walimu 8 wa Kiswahili katika vyuo vikuu. Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu la kubainisha makosa ya kimofofonolojia ya kimatamshi na kimaandishi ya Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wanaoongea Kirundi (L1). Malengo mahususi katika utafiti huu ni matatu yaani (1) kubaini athari za kimofofonolojia za Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi zinazojitokeza katika kazi zao((2)) kutathmini viwango vya utamalaki wa aina mbalimbali za athari zaa kimofofonolojia Kirundi katika ujifunzaji wa kiswahili

kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi; na (3) kubainisha juhudi za walimu kubaini na kukabiliana na aina bainishwa za athari. Mbinu za kukusanyia data zilikuwa hojaji, ushuhudiaji na jaribio la umilisi. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa msingi wa kinadharia wa Uchanganuzi Linganuzi (UL). Michakato ya usampulishaji iliyotumiwa ni miwili, yaani usampulishaji usio nasibu na usampulishaji nasibu. Data zilizokusanywa zilitolewa maelezo, zilichambuliwa na kufupishwa kwa kutumia mkabala wa kiidadi  na wa kimaelezo. Katika utafiti huu, mtafiti alizingatia maadili ya kupata kibali cha kufanya utafiti, kutunza siri za watafitiwa kwa kuhifadhi na kutosambaza habari zinazowahusu na ambazo hawakupenda ziwe hadharani, kuheshimu mipaka ya utafiti kabla na baada ya kukusanya data ili afikie malengo ya utafiti huu kwa ufanisi mkubwa.

### 5.2.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yalitokana na malengo ya utafiti huu.

Lengo la kwanza lilikuwakubaini athari za kimofofonolojia za Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2) kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi zinazojitokeza katika kazi zao, na lengo la pili lilikuwa kutathmini viwango vya utamalaki wa aina mbalimbali za athari   zaa kimofofonolojia Kirundi katika ujifunzaji wa kiswahili kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi; na (3) kubainisha juhudi za walimu kubaini na kukabiliana na aina bainishwa za athari..

Kwa upande wa malengo ya kwanza na pili, imebainika kuwa athari za kimofofonolojia ya Kirundi zimeibuka katika kazi zote za Kiswahili za wanafunzi watafitiwa wetu. Athari hizi zilihusu  michakato ya kimofofonolojia mikuu mitatu yaani utumiaji wa uchopekaji, udondoshaji naubadilishanaji wa fonimu.

Baadhi ya wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi (L1) wanaojifunza Kiswahili (L2) huchopeka sauti mojawapo miongoni mwa /i/, /u/, /h/, /j/, /w/ pia hudondosha baadhi ya sauti wakati wazungumzapo au waandikapo lugha ya Kiswahili, sauti ambayo ilidondoshwa mara nyingi ni /h/, yaani kwa 10.01%, hasa ilipotokea katika sauti mwambatano. Tatizo la utamkaji wenye kasoro limehamishiwa katika maandishi ya maneno husika; mfano maneno ***amsini**, ***luga**. Neno ***luga** linadhihirisha kudondoshwa kwa sauti /h/ ambayo inatakiwa kutokea baada ya /g/ ili kuunda sauti /ɣ/. Pamoja na hayo, ilibainika makosa ya matumizi ya ubadala yaliyotokana na ukweli kwamba katika lugha ya Kiswahili kuna sauti ambazo hazipo katika lugha ya Kirundi. Wanafunzi husika walitumia sauti wanazozifahamu katika L1; na hivyo kuleta kasoro katika maneno ya Kiswahili kimatamshi na kimaandishi. Uchambuzi wa data ulidhihirisha jumla ya makosa 1018 yaliyogawanyika katika makundi makuu matatu ya athari za kimofofonolojia, yaani athariza kimofofonolojia za mchakato wa uchopekaji yalijitokeza kwa kiasi cha 405 sawa na 39.78%, athari za kimofofonolojia za mchakato wa udondoshaji kwa kiasi cha 102 sawa na 10.01%, na za mchakato wa ya matumizi mbadala kwa kiasi cha 511 sawa na 50.19%. Uchanganuzi huu umebainisha kuwa nyingi za athari za kimofofonolojia ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2)kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi wa baadhi ya vyuo vikuu nchini Burundi hutokana na mifumo ya isimu ya L1 yao.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kubainisha juhudi za waalimu kubaini na kukabiliana na aina za athari za Kimofofonolojia ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi. Uchunguzi na uchanganuzi wa data ulionyesha kuwa mbinu walimu watafititiwa walizoainisha ni za hatua kwa hatua kufuatana na stadi kuu nne za ufundishaji wa lugha, yaani kusikiliza,

kuzungumza, kusoma na kuandika. Ili kupunguza athari za kimofofonolojia za lugha ya Kirundi (L1) katika ujifunzaji wa Kiswahili (L2), walimu watafitiwa walieleza kwamba wanawazoesha wanafunzi kusikiliza,kuongea, kusoma na kuandika Kiswahili.

Utafiti huu umedhihirishia kwamba maswali ya utafiti huu yana mashiko. Aidha, mtafiti ameweza kuthibitisha kwamba athari za kimofofonolojia za Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi zipo kutokana na michakato ya kimofofonolojia mtafiti aliyoorodhesha. Mtafiti alidai kwamba tofauti zilizopo baina ya fonimu na miundo silabi za Kiswahili na Kirundi husababisha lugha ya Kirundi kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi.

### 5.3 Hitimisho la Sura ya Tano

Mtafiti amechanganua makosa ya kimofofonolojia yanayoibuka kwa wanafunzi wa Kiswahili (L2) wazungumzaji wa Kirundi (L1). Utafiti huu umebainisha kuwepo kwa usukukukaji wa Kirundi (L1) katika uamiliaji wa Kiswahili (L2). Kazi za Kiswahili za wanafunzi hawa zinakumbwa na makosa ya kimofofonoljia. Imebainika wazi kuwa mengi ya makosa ya kimofofonolojia katika uamiliaji wa L2 hutokana na kuwa L1 na L2 hutofautiana kiisimu. Hivyo wanapoamili L2 hukumbana na mfumo wa fonimu na miundo ya silabi migeni kwao. Hali hii husababisha wanafunzi wa L2 kuhawilisha mifumo ya isimu ya L1 yao hadi L2. Makosa kama haya ni sharti yaibuke katika ujifunzaji wa L2 lakini yafaa yaangaliwe kama mkakati wa mtu kuimudu sarufi ya L2.

### 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu hauwezi kudai kwamba umeshughulikia athari za Kimofofonolojia za Kirundi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa jamiilugha ya Kirundi kikamilifu.Kwa sababu hii tunapendekeza haya yafuatayo.

#### 5.4.1 Mapendekezo ya kiutekelezaji kwa watunga muhtasari wa somo, watunga sera za lugha katika elimu, kwa walimu

Kiswahili ni lugha ya kimataifa ambayo inapaswa kupewa kipaumbele katika orodha ya masomo yafundishwayo nchini Burundi. Kwa hiyo, mapendekezo yafuatayo yafaa kutolewa.

Kwanza, kwa serikali, kutunga na kuweka sera inayoipa kipaumbele lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, kuanzia shule za msingi hadi vyuoni. Aidha, Serikali iwawezeshe walimu wa Kiswahili kujiandaa na kupata mafunzo maalumu kuhusu ufundishaji wa lugha ya Kiswahili ili kupata uwezo wa kufundisha kwa ufanisi. Serikali inatakiwa pia kuandaa vitabu vya kutosha vinavyowasaidia walimu na wanafuzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Pili, kwa watunga mitaala, hawa wanapaswa kuandaa masomo ambayo yanalingana kabisa na kiwango cha elimu husika.

Tatu, kwa walimu, nchini Burundiuamuzi wa kufundisha lugha ya Kiswahili katikaa ngazi zote za elimu ni jambo jipya, walimu wanapaswa kufanya bidii katika kujitafutia wenyewe maarifa yanayohusiana na lugha ya Kiswahili na ufundishaji wa lugha hiyo. Aidha, waimarishe ushirikiano ili kuendelezana kitaaluma. Kwa upande

wa walimu wa vyuo vikuu na vyuo vya kati, wanatakiwa kuwa na ujuzi wa kutosha katika taaluma za isimu na hata fasihi ya Kiswahilli ili waweze kusaidia wanachuo katika utumiaji bora wa lugha ya Kiswahili.

### 5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti Zitakazokuja

Utafiti huu ulilenga kutathmini athari za mofofonolojia za lugha ya Kirundi (L1) katika uamiliaji wa Kiswahili (L2). Kazi hii ilibaini kuwa, mara nyingi, wanafunzi wa Kiswahili (L2) hufanya makosa kutokana na muundo wa kiisimu waliozoea, yaani muundo wa Kirundi, L1 yao. Hivyo, tafiti fuatishi zifanyike kwa mfano, kuchanganua makosa katika nyanja zingine za isimu kama mofosintaksia, pragmatikia, sintaksia, semantikia, nathari kwa wazungumzaji wa Kiswahili wa mjini na vijijini, n.k. Aidha, tafiti zingine zifanyike kama tafiti linganishi katika nafasi ya jinsia na kiwango cha elimu katika kuathirika na L1.

## MAREJELEO

Bamporubusa, M. (2012). Matatizo Yanayojitokeza katika Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili Sanifu katika Ngazi ya Pili ya Shule za Msingi Nchini Burundi. Tasnifu ya Shahada ya kwanza (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Burundi. Bujumbura.

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Bryman, A. (2004). *Elements of Education and Social Science Research Methods*. Masola Publishers.

Chomsky, N. (1976a). Conditions on rules of grammar. *Linguistic Analysis* 2: 303–351. New York: Plenum Press.

Chaochuan, Y. (2005). *Second Language Learning: Conscious or Unconscious*? *CELEA* 28(4): 24-31.

Cohen, L. (2007). *Research Methods in Education (5th ed)* London: Rontledge.

Corder, S. P. (1967) *Error Analysis and Interlanguage.*Oxford: Oxford University Press.

------------. (1973). *Introducing applied linguistics*. Harmondsworth: Penguin Education.

------------. (1975). *Error Analysis, Interlanguage and Second Language Acquisition.* Cambridge: Cambridge University Press

-------------. (1983). "A Role for Mother Tongue" in Gass, S.and Selinker. L. (wahariri) *Language in Learning* . Rowley:Newbury House.

-------------.(1967).The Significance of Learner's. Error. *International Review of Applied Linguistics* 5: 161-170.

Ellis, R. (1985*). Understanding Second Language Acquisition*. Oxford: OUP.

---------. (1996). *The Study of Second Language Acquisition.* Oxford: OUP. *Encyclopedia of Language and Linguistics* (2nd ed.) UK. 3276-3286. Elsevier Ltd.

Enon, J. C. (1998). Education Research, statictics and Measurement. Unpublished. MA. Dissertation, Makerere University.

Fletcher, P. & Garman, M. (1986). *Language Acquisition*. Cambridge: Cambridge University Press.

Fromkin, V., Rodman, R., na Hyams, N. (2007). *An Introduction to Language (8thed.)*. Boston, MA: Thomson Wadsworth.

Gass, S. & L.Selinker (2008*). Second Language Acquisition: An Introductory Course*. New York: Routledge.

Gathumbi, A. & Masembe, S. (2005). *Principles and Techniques in Language Teaching*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Gleason, J. B. (1989). *The Development of Language* (2nd ed.). Columbus, OH: Merrill. Published online by Cambridge University Press:28 November 2008

Haroon, M. B. (1998). *Kuathiriana kwa Kigisu na Kiswahili*. Tasnifu ya Diploma ya Juu, Ndaki ya Kiisilamu nchini Uganda, Mbale-Uganda.

Habwe, J. & Karanja, P. (2007). *Msingi wa Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Iribemwangi, P. (2010). *The Structure of Kiswahili Sounds, Sound changes and Words*. Saarbruken: Verlag

Irakoze, S.J. (2015). The impact of English on Kirundi and French in Burundi: Use and Attitudes among Burundian Students. M.A Dissertation in Language Studies, University of Tlemcen.

Kihore, Y, Massamba, D., Matangila, M. (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Kombo, D. K., & Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, R. C. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. 2nd Edition. New Delhi: Wiley Easton Limited.

--------------. (2008), *Research Methodology; Methods.* New Delhi New Age. International Publishing LTD Techniques.

----------------. (2014). *Research Methodology, Methodes and Techniques.* 3rd edition, New Delhi: New age International (P) Ltd.

Krashen, D.S. (1981). *Second Language Acquision and Second Language Learning*. Oxford: Pergamon Press.

Krashen, D. S. & Tracy, D. T. (1983). *The Natural Aproach Language Acquisition in The Classroom.* Oxford:Pergamon Press.

Lado, R. (1957). *Linguistics across Cultures: Applied Linguistics for Language Teachers*. Ann Arbor: University of Michigan Press.

Mashaka, W. (2015).Athari za Lugha ya Kijita Katika Kujifunza Kiswahili. Tasnifu ya uzamili(Haijachapishwa), M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massamba, D. P. B. (2016). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI,

-------------------. (1986). On the Influence of Local Languages on Kiswahili: The case of Mara Region in Tanzania.*Kiswahili,* 53(1): 67-83

--------------------. (2009) *Sarufi Miundo ya Kiswahili.*Dar es Salaam:TUKI.

Mbonabuca, P.D. (2019). A strong influence of Kinyarwanda on Kirundi. Study: Burundians Living in Rwanda. Dissertation for the Kibungo. Rwanda.

Mlingo E.S. (2012). *Jifunze Utafiti Mwongozo kuhusu Utafiti na Utamaduni wa Ripoti yenye Mantiki*. Dar es Salaam. Ecumenical Gathering (EGY)

Mpangala, G. (2019). Athari ya Lugha ya Kimakonde katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya uzamili(Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria chaTanzania.

Msanjila, Y. P. (2009). *Isimu Jamii.Sekondari na Vyuo*. Dar es salaam: TUKI.

Mtugu, B.N. (2001). Makosa ya Kileksia katika Insha na Chanzo chake: Uchunguzi wa Shule Tano za Upili Wilayani Kiambu. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mukuthuria, M. M.A. (2004).Kuathiriana Kwa Kiswahili Na Kimeru: Mfano Kutokana na wanafunzi wa Tigania, Kenya.Tasnifu ya Uzamili. (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Egerton – Kenya.

Munyua, J. G. (2002). “The Emerging Viswahili and Kiswahili Research”. Ktk K. I. Simala (Mh.) *Jarida la Utafiti wa Kiswahili* (kur. 97 – 107). Eldoret: Moi University Press.

Ndung’u, I. (1999) Kikuyu Learners of English as Second language: PhD. Thesis*:*University of Nairobi.

Ngugi, J. K. (2007). Uchunguzi wa Taathari za Kifonolojia miongoni mwaWanafunzi Wagikuyu: Mfano kutoka Tarafa ya Bahati, Nakuru.

Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya Nickel, G. (1971 ). *Contrastive Linguistics and Foreign Language Teaching*. In Nickel, G. (ed.), *Papers in contrastive linguistics*. London: CUP.

Niyonizeye, J.B. (2013). Changamoto za Utumiaji wa Lugha ya Kiswahili Sanifu Nchini Burundi: Tarafani Kamenge. Tasnifu ya Shahada ya kwanza (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Burundi. Bujumbura.

Niyubahwe, B. (2017). Makosa Yanayojitokeza katika Vitabu Vya Kiswahili vya Shule za Msingi Nchini Burundi. (Kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la tisa). Tasnifu ya Shahada ya kwanza (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Burundi. Bujumbura.

Njoroge, M. (1996) Morphosyntactic Errors in the Written English of First Year Undergraduate Students in Kenya. Unpublished M. A Thesis, Kenyatta University.

Ntawiyanga, S. (2015). Changamoto za Kimofosintaksia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Shule za Upili Wilayani Muhanga, Nchini Rwanda. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nyanda, J. (2015*)* Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili Eneo la Utafiti: Urambo. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Onyango, J.O. (1997). Uziada wa Kisarufi katika Kiswahili cha Wanafunzi wa Kinyala Mtazamo wa Uchanganuzi Linganuzi. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). huo Kikuu cha Kenya.

Otiende, M. A. (2013). Athari za Mofofonolojia ya Kibasuba katika Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya Pili.Tasnifu ya uzamili(Haijachapishwa). M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Rapando, M.M. (2005). Makosa ya kimofosintaksia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili Jijini Nairobi. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi .

Richards, Jack C. and Rodgers, Theodore S. (1986). *Approaches and Methods in Language Teaching*. Cambridge: Cambridge University Press.

Saville-Troike**,** M. (2006). *Introducing Second* Language Acquisition. London: Cambridge University Press.

Selinker, L. (1969) *Language Transfer, General Linguistics*. New York: Rawlence Eribaum Associates, inc. (RAL).

Selinker, L.(1972) *Interlanguage*. New York: Rawlence Eribaum Associates, inc. RAL.

Sigh K. (2007). *Research Methodology; Methods.* New Delhi: Sage publication

Stern, H. H. (1983). *Fundamental Concepts of Language Teaching*. Oxford: Oxford University Press.

UNESCO. (2003). *Education in a Multilingual World*. Paris UNESCO (Education Position Paper) htt: //unesdoc.unesco.org/ images /0012/001297/ 129728e. pdf. Accessed 25th September 2018.

Van Patten, B.na Williams, J. (Wah.)(2015). *The Theories in Second Language Acquisition: An Introduction.* New York: Routledge.

Were, E. A. (1996). First Language Influence on Kiswahili Composition Writing:

The Case of Bukusu Students of Kanduyi, Bungoma. Unpublished M. A. Thesis. Kenyatta University, Nairobi.

Wilkins, R. (1972).*The Second Language Acquisition.* Retrived 28, 2014 from http:www. cdc.eun.eg/en.htm.

Yin, R.K (1994). *Case Study Research Design and Methods (2ndeds);* ThousandOaks Calif:Sage Publishers.

## VIAMBATISHO

**HOJAJI KWA WANAFUNZI**

Mimi ni BIZIMANA Jean, mwanafunzi wa MA- Isimu ya Kiswahili katika Chuo Kiku Huria Cha Tanzania. Ninafanya Utafiti kuhusu“ Athari za mofofonolojia za Kirundi Katika uamiliaji wa Kiswahili kama lugha ya pili”. Kazi hii ni kwa ajili ya kitaaluma. Hii ni sehemu ya mahitaji ya kukamilisha masomo yangu ya Shahada ya Uzamili. Hivyo ninaomba ushirikiano wako wa kujibu maswali haya ili yasaidie kukamilisha utafiti huu.Toa habari za kweli bila woga wowote.Usiandike jina lako.Habari zozote zitashughulikiwa kama siri na zitatumika kwa utafiti huu tu.Ninatanguliza shukurani za dhati kwa ushirikiano wako.

**SEHEMU A**

Maswali: Tumia alama X kuonyesha jibu unaloliona ni sahihi.

1. Umri wako (age)

a) 15-20 b) 20 – 25 c) 25 – 30 d) 30 na zaidi

2. Jinsia (gender)

a) Mwanamke b) Mwanamke

3. Kiwango cha elimu

a) Elimu ya sekondari b) Elimu ya chuo kikuu

1. Lugha yako ya kwanza ni

(a) Kiswahili (b) Kirundi

2. Shuleni unapendelea kutumia lugha gani?

(a)Kirundi (b) Kiswahili

Jibu lolote utakalolichagua eleza sababu za kuchagua lugha hiyo;

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

3. Mwalimu anakusaidiaje darasani unapotumia Kirundi wakati wa kujifunza Kiswahili? Eleza kwa kifupi

------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------

4. Unapokuwa nyumbani unapendelea kutumia lugha gani kufanya mawasiliano na rafiki zako?

(a) Kirundi (b) Kiswahili

**SEHEMU B: MASWALI YA IMLA**

Andika kama unavyosikia

1. Cha mlevi huliwa na mgema
2. Nguo za watoto huhifadhiwa
3. Fungua mlango na dirisha.
4. Mzee Kasorogani amesema kwamba ataoga mwaka ujao.
5. Kioo cha bibi harusi kilianguka na kuharibika vibaya.
6. Nauli ni fedha inayolipia gharama ya safari.
7. Chajio ni chakula kinacholiwa jioni.
8. Endelea ninaipenda hadithi hiyo !
9. Maktaba ni mahali ambapo vitabu na vifaa vinavyohusika na elimu vinahifadhiwa ili wasomaji wavitumie.

**SEHEMU C:  KUANDIKA INSHA**

Andika insha juu ya mvua iliyonyesha sana wakati huu wa masika.

**SEHEMU D**: Kama mlivyofundishwa salamu mbalimbali za adabu na heshima katika lugha ya Kiswahili kama vile salamu kwa watu wazima, kwa watu wenye rika sawa, kwa watu wadogo pamoja na salamu za kujitambulisha; igizeni namna ya kusalimiana. Kazi hii ifanyike katika makundi ya wanafunzi wanne wanne.

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**VIAMBATISHO II**

**HOJAJI KWA WALIMU WANAOFUNDISHA SOMO LA KISWAHILI**

Mimi ni BIZIMANA Jean, mwanafunzi wa MA- Isimu ya Kiswahili katika Chuo Kiku Huria Cha Tanzania. Ninafanya Utafiti kuhusu" Athari za mofofonolojia za Kirundi Katika uamiliaji wa Kiswahili kama lugha ya pili". Kazi hii ni kwa ajili ya kitaaluma. Hii ni sehemu ya mahitaji ya kukamilisha masomo yangu ya Shahada ya Uzamili. Hivyo ninaomba ushirikiano wako wa kujibu maswali haya ili yasaidie kukamilisha utafiti huu.Toa habari za kweli bila woga wowote.Usiandike jina lako.Habari zozote zitashughulikiwa kama siri na zitatumika kwa utafiti huu tu. Ninatanguliza shukurani za dhati kwa ushirikiano wako.

Umri.............................................................................Ujinsia ..................................

Kiwango cha Elimu.........................................................................................................

**MASWALI**

**SEHEMU A**: Tumia alama X kuonyesha jibu lako

1. Unavyojifahamu wewe mwenyewe, unahisi weledi wako kama mwalimu wa kuzungumza na kuelewa Kiswahili ni wa kiwango gani?

a) Mzuri sana

b) Mzuri

c) Kiasi

d) Mbaya

e) Mbaya sana

2. Ni kwa kiwango gani unakubali kwamba wanafunzi katika shule yako wanaathiriwa na Kirundi katika matumizi na kazi zao za Kiswahili?

a) Ninakubali kabisa

b) Ninakubali

c) Sikubali

d) Sikubali kabisa

3) Ni kwa kiwango gani unakubali kwamba matokeo ya kazi zao katika somo la Kiswahili yanaridhisha?

a) Ninakubali kabisa

b) Ninakubali

c) Sikubali

d) Sikubali kabisa

**SEHEMU B**

1. Wanafunzi unaowafundisha wana uwezo wa kuzungunza na kuandika Kiswahili fasaha?

(a) ndiyo (b) hapana

2. Je, lugha ya Kirundi inaathiri wanafunzi wanapojifunza lugha ya Kiswahili sanifu?

(a) ndiyo (b) hapana

3. Je, kuna sababu zinazochangia kuathiriwa kwa wanafunzi wa Burundi katika kuamili Kiswahili kama lugha yao ya pili?

(a) ndiyo (b) hapana

Ikiwa jibu lako ni “ndiyo”, onyesha sababu za athari hizo kutoka katika orodha ifuatayo kisha ongeza zisizoorodheshwa hapa. Andika ‘Vyema’ au ‘La’.

(i) Mfuatano wa fonimu irabu, usiokubalika katika lugha ya Kirundi, ambao ni wa kawaida katika lugha ya Kiswahili. → ………………

(ii) Mfuatano wa fonimu konsonanti usiokubalika katika lugha ya Kirundi, ambao ni wa kawaida katika lugha ya Kiswahili. → ……………

(iii) Uwepo wa silabi funge katika Kiswahili ambao si wa kawaida katika Kirundi.→……….

(iv) Uwepo wa baadhi ya fonimu za Kiswahili ambazo si za asili katika Kirundi. →……..

(v) Uhamishaji wa baadhi ya kanuni za kiisimu za Kirundi hadi lugha ya Kiswahili. → …………

4. Je, wewe kama mwalimuwa Kiswahili, Unakabiliana na changamoto wakati unapowafundisha wanafunzi wa Burundi lugha ya Kiswahili?

(a) ndiyo (b) hapana

Ikiwa jibu ni ndiyo, katika orodha ifuatayo, onyesha changamoto ipi /zipi unakutana nazo darasani unapofundisha Kiswahili wanafunzi wa Burundi. Andika ‘Vyema’ au ‘La’. Kisha ongeza zisizoorodheshwa hapa.

(i) Kufundisha wanafunzi wazima ambao lugha mama si Kiswahili. → ………

(ii) Kuiona lugha ya Kiswahili kama lugha ya wahuni na wasio na thamani. → ……

(iii) Kutokuwa mwelevu katika kuamili Kiswahili. → ………

(iv) Uwanja wa kifonolojia ambapo Kiswahili hutofautiana na Kirundi. → ………

(v) Uwepo wa uwanja wa kimofolojia ambapo Kiswahili kinatofautiana na Kirundi. → …………

(vi) Kutofautiana kwa kanuni za upatanisho wa kisarufi kati ya Kiswahili na Kirundi. → …………

5. Je, kuna mbinu unazotumia ili kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na athari za Kirundi wakati wa kujifunza lugha ya Kiswahili?

(a) ndiyo (b) hapana

Ikiwa jibu ni 'ndiyo', katika orodha ifuatayo, onyesha mbinu unazotumia ili kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na athari za Kirundi wakati wa kujifunza lugha ya Kiswahili. Andika 'Vyema' au 'La'. Kisha ongeza zisizoorodheshwa hapa. .

(i) Katika stadi ya usikivu, mbinu unazotumia ni:

1°) Mbinu ya Kusoma aya fupifupi na kuuliza wanafunzi maswali ya ufahamu. → …

a) Kuomba wanafunzi waandike katika madaftari yao kile walichosikia. → ……

b) Kuomba kila mwanafunzi asome alichoandika. → ……

c) Kuandika ubaoni makosa yaliyojitokeza kutokana na miundo ya maneno na sauti zinazowatatiza. → ……

d) Kurekebisha makosa na kuwaambia wanafunzi mmoja mmoja kusoma kwa usahihi maneno yaliyoandikwa ubaoni. → ……

2°) Mbinu ya kusoma aya nzima na kuuliza wanafunzi maswali ya ufahamu. → ……

a) Kuhakikisha matamshi ya maneno. → ………

b) Kurekebisha makosa panapohitajika. → ………

3°) Mbinu ya kusoma matini polepole (kama imla) na wanafunzi wanaandika. → ……

a) Kuambia wanafunzi kusoma kwa sauti. → ……

b) Kuandika ubaoni makosa ya kimatamshi yaliyojitokeza wakati wa kusoma. → …

c) Kuwaambia wanafunzi kurekebisha makosa. → ……

d) Kuwaambia wanafunzi wasome sentensi ziandikwazo ubaoni ili matamshi ya maneno yawe sawasawa. → ……

(ii) Katika stadi ya uzungumzaji, mbinu unazotumia ni:

1° Kuwaambia wanafunzi wasimulie habari katika lugha ya Kiswahili na kisha wewe mwalimu ukaandika ubaoni makosa ya mofofonolojia ya kimatashi wanayofanya.

→ ……

2° Kupitia kosa moja baada ya jingine na kuwaomba wanafunzi kusahihisha. → …

3° kuandika usahihi wa maneno ubaoni na kuwaomba wanafunzi kuyasoma kwa usahihi. → ……

(iii) Katika stadi ya usomaji, mbinu unazotumia ni:

1° kuwapa wanafunzi kazi ya kusoma na kufahamu habari. → ……

2° kuwauliza maswali ya ufahamu. → ……

3° Kuwaambia wataje maneno magumu, kuyaandika ubaoni na kuwauliza maana zake. → ……

4° Kuwaambia wasome tena habari kwa sauti na Kuandika ubaoni makosa ya matamshi. → ……

5° Kurekebisha makosa yaliyofanywa na wanafunzi wakati waa kusoma. → ……

(iv) Katika stadi ya uandishi, mbinu unazotumia ni:

1° Kuwaambia wanafunzi kuandika habari kuhusu mada fulani. → ……

2° Kumwomba kila mwanafunzi asome habari aliyoandika. → ……

3° Kuandika ubaoni makosa yaliyojitokeza na kuorodhesha maneno yenye sauti zinazowatatiza kimatamshi au kimaandishi. → ……

4° Kuyarekebisha makosa yote na kuwaambia wanafunzi wayasome na kuyaandika kwa usahihi. → ……

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO !**